

*Mheshimiwa Kaspar Kaspar Mmuya, Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi akitatua mgogoro wa ardhi wakati wa Kliniki ya Ardhi jijini Dodoma*

KIMEPIGWACHAPA NA MPIGACHAPA MKUU WA SERIKALI, DODOMA-TANZANIA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**

# HOTUBA YA WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI MHE. DKT. LEONARD AKWILAPO (MB.) AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA 2026/27



**Imeandaliwa na:**
Wizara ya Ardhi, Nyumba
na Maendeleo ya Makazi
S. L. P. 2908,
**40477-DODOMA**

**Mei, 2026**




*Mhandisi Anthony Sanga, Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi akikagua alama ya mpaka wa Kimataifa kati ya Tanzania na Kenya, eneo la Holili mkoani Kilimanjaro*




*Bi. Lucy Kabyemera, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (katikati) akishuhudia mkazi wa Dar es Salaam akikabidhiwa Hati wakati wa Samia Ardhi Kliniki*

## VIONGOZI WA WIZARA



MHE. DKT. LEONARD DOUGLAS AKWILAPO (MB.)
**WAZIRI**



MHE. KASPAR KASPAR MMUYA (MB.)
**NAIBU WAZIRI**



Eng. ANTHONY SANGA
**KATIBU MKUU**



Bi. LUCY KABYEMERA
**NAIBU KATIBU MKUU**

## YALIYOMO

**UTANGULIZI ........................................... 5**

**SALAMU ZA PONGEZI ................................ 6**

**SALAMU ZA POLE .................................... 10**

**MAJUKUMU YA WIZARA ........................... 11**

**MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2025/26 NA MALENGO YA MWAKA 2026/27 ................................................. 15**

Mapato na Matumizi ya Fedha (Fungu 48)... 15

***Mapato* ................................................. 15**

***Matumizi* ............................................ 17**

Mapato na Matumizi ya Fedha: Fungu 03.... 18

***Mapato* ................................................. 18**

***Matumizi* ............................................ 19**

**UTAWALA WA ARDHI ............................... 20**

Uandaaji na Usajili wa Hati na Nyaraka za Kisheria ................................................... 20

Usimamizi wa masharti ya umiliki............... 23

Usimamizi wa Ardhi ya Uwekezaji ............... 24

Uhuishaji wa Kumbukumbu za Ardhi.......... 26

Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi Kiutawala ..... 28

Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi katika Vijiji/Mitaa 975 .......................................... 31

**Uthamini wa Mali ................................... 32**

**MABARAZA YA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA............................................... 35**

**HUDUMA ZA TEHAMA ............................. 36**

**UPIMAJI ARDHI NA UTAYARISHAJI WA RAMANI ................................................ 38**

Uwekaji Alama za Msingi za Upimaji Ardhi .. 39

Upigaji Picha za Anga ................................ 40

Tafsiri ya Matangazo ya Serikali kuhusu Maeneo ya Utawala (GN)............................ 41

Upimaji wa Viwanja na Mashamba............. 42

Upimaji wa Mipaka ya Vijiji ....................... 43

**UPANGAJI MIJI NA MAENDELEO YA MAKAZI ................................................ 43**

Utangazaji wa Maeneo ya Upangaji Miji ....... 44

Uandaaji wa Mipango ya Jumla.................. 45

Uandaaji wa Mipangokina .......................... 46

Urasimishaji Makazi................................... 47

Udhibiti wa Uendelezaji Miji ....................... 48

Uendelezaji Upya na Uboreshaji wa Maeneo Chakavu Mijini.......................................... 49

Usimamizi na Uratibu wa Uendelezaji Nyumba ................................................... 51

Mikopo ya Ujenzi wa Nyumba...................... 52

Ushirikiano na Taasisi za kimataifa Katika Uendelezaji wa Makazi ............................... 53

**USIMAMIZI NA URATIBU WA SEKTA YA MILKI ..................................................... 56**

**MAPITIO YA SHERIA ZA SEKTA YA ARDHI ................................................... 58**

**MIRADI YA MAENDELEO......................... 58**

Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi.......................................................... 59

Mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu ya Upimaji na Ramani .............................................. 60

Mradi wa Uimarishaji wa Mipaka ya Kimataifa ................................................... 62

**TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA .......... 66**

**Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi............................................... 66**

Uandaaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi........................................................ 68

Uandaaji wa Mipangokina .......................... 70

Kuzijengea Uwezo Mamlaka za Upangaji...... 71

Ufuatiliaji na Tathmini ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi........................................................ 73

**Shirika la Nyumba la Taifa ...................... 74**

**BODI ZA USAJILI WA WATAALAM WA FANI ZA ARDHI ........................................ 84**

**Bodi ya Usajili wa Wataalam wa Mipangomiji............................................. 85**

**Bodi ya Usajili wa Wathamini ................. 86**

**Bodi ya Usimamizi na Usajili wa Wapima Ardhi ......................................... 87**

**VYUO VYA ARDHI TABORA NA MOROGORO............................................. 88**

**UTAWALA NA RASILIMALIWATU.............. 91**

**HABARI NA ELIMU KWA UMMA ............... 95**

**SHUKRANI ............................................ 99**

## UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika***, naomba kutoa hoja kwamba, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii iliyochambua na kujadili Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu **48**) na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu **03**), Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu **48**) na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu **03**) kwa mwaka 2025/26. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mafungu hayo mawili kwa mwaka 2026/27.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kushiriki Mkutano wa Tatu wa Bunge la **13** ambao ni mahsusi kwa ajili ya kujadili Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2025/26 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2026/27. Aidha, kipekee namshukuru **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo

ya Makazi. Ninamuahidi kuwa kwa kushirikiana na viongozi na watumishi wote wa Wizara nitaendelea kutekeleza majukumu aliyonikabidhi kwa uadilifu na weledi ili kuleta ufanisi katika utoaji wa huduma katika Sekta ya Ardhi kwa ustawi wa wananchi na maendeleo ya Taifa kwa ujumla. Vilevile, namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kunipatia Msaidizi makini, mahiri na mchapakazi Mheshimiwa Kaspar Kaspar Mmuya (Mb.), Naibu Waziri ambaye amekuwa akinisaidia katika kutekeleza majukumu ya sekta.

**SALAMU ZA PONGEZI**

3. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya pekee naomba nitumie fursa hii kumpongeza kwa dhati **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa ushindi wa kishindo alioupata katika Uchaguzi Mkuu uliofanyika Oktoba, 2025. Ushindi huo ni ishara ya imani waliyonayo Watanzania kutokana na uongozi mahiri wa Serikali ya Awamu ya Sita ambao umedumisha amani, umoja, upendo na mshikamano nchini; umeimarisha utulivu wa kisiasa na diplomasia ya uchumi; na kuvutia uwekezaji katika sekta ya ardhi na uendelezaji milki. Miongoni mwa masuala makubwa yaliyofanywa na Mheshimiwa Rais katika sekta ya ardhi kwa kipindi cha uongozi wake ni pamoja na kuwezesha ukamilishaji wa marekebisho ya Sera ya Taifa ya Ardhi ya

mwaka 1995 hivyo kuwa na Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 (Toleo la mwaka 2023) ambayo imetoa mwelekeo mpya wa usimamizi wa ardhi nchini. Aidha, Mheshimiwa Rais amewezesha maboresho ya mifumo ya TEHAMA na upatikanaji wa rasilimali kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za sekta ya ardhi nchini.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** nampongeza Mheshimiwa Balozi, Dkt. Emmanuel John Nchimbi kwa kuaminiwa na kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, nampongeza kwa umahiri wake katika kuendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais kutekeleza majukumu yake ya kuliongoza Taifa letu. Ninamshukuru kwa maelekezo na miongozo ambayo imeendelea kuniwezesha kutekeleza majukumu ya kuongoza sekta hii muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** nampongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa uongozi mahiri kwa kuendelea kudumisha misingi ya Muungano pamoja na kusimamia maslahi na ustawi wa wananchi wa Zanzibar.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** nampongeza Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb.) kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais na kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Namshukuru kwa hotuba yake ambayo imetoa mwelekeo wa utekelezaji wa shughuli za sekta ya ardhi. Miongoni mwa masuala yaliyotiliwa mkazo katika hotuba hiyo ni pamoja na kusimamia upangaji na upimaji wa ardhi mijini, vijijini na maeneo ya kimkakati; kuimarisha mifumo ya TEHAMA; kuboresha huduma za uthamini na ulipaji fidia; kuimarisha mifumo ya utatuzi wa migogoro; kuendeleza ujenzi wa nyumba za gharama nafuu; na kuboresha miundombinu ya upimaji na ramani ili kuongeza tija, uwazi na kasi ya utoaji huduma. Wizara imezingatia na inaendelea kutekeleza maelekezo na maagizo yanayohusu sekta ya ardhi ili kuimarisha usalama wa milki za ardhi nchini, kudhibiti migogoro ya ardhi, kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji na kuifanya ardhi kuwa mtaji hai kwa wananchi.

7. ***Mheshimiwa Spika***, napenda kukupongeza wewe binafsi kwa kuaminiwa na kuchaguliwa kuliongoza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Daniel Baran Sillo (Mb.) kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania. Vilevile, ninawapongeza wenyeviti wa Bunge Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum; na Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini ambao kwa nyakati tofauti wamekuwa wakisimamia na kuongoza shughuli za Bunge. Tunawaombea kwa Mwenyezi Mungu aendelee kuwajalia afya njema na hekima katika kuwatumikia wananchi kupitia Mhimili huu wa Bunge.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya pekee natoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii chini ya uongozi mahiri wa Mwenyekiti Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava (Mb.) kwa maoni na ushauri ambao umeiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Pia, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati kwa uchambuzi makini wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara (Fungu **48**) na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu **03**) kwa mwaka 2026/27. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati yamezingatiwa katika bajeti hii na hivyo kutoa mwelekeo mpya wa utekelezaji wa shughuli za Sekta ya Ardhi.

**SALAMU ZA POLE**

9. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa salamu za pole kwa **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa msiba mzito wa kuondokewa na Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Isimani na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu) uliotokea tarehe 25 Machi, 2026 katika Hospitali ya Benjamin Mkapa, jijini Dodoma. Mheshimiwa Lukuvi atakumbukwa kwa mchango wake mkubwa katika kujenga misingi ya utawala bora na maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini. Aidha, atakumbukwa kwa kuweka misingi madhubuti ya utawala na usimamizi wa sekta ya ardhi kwa kipindi alichohudumu kama Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuanzia mwaka 2015 hadi 2022.

10. ***Mheshimiwa Spika,*** naungana na waheshimiwa wabunge wenzangu kutoa pole kwako wewe binafsi na Bunge lako Tukufu kutokana na kifo cha Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Peramiho na Mheshimiwa Halima Idd Nassor aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum. Aidha, natoa pole kwa familia za marehemu, ndugu, jamaa na wananchi walioguswa na misiba hiyo. Vilevile, wapo viongozi na Watanzania wenzetu

waliofikwa na ajali, majanga na maafa mbalimbali yaliyosababisha vifo, majeruhi na uharibifu wa mali. Nitumie fursa hii kuwapa pole wote waliopoteza ndugu, jamaa, marafiki na mali zao kutokana na maafa hayo. Tunamuomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu wote mahali pema peponi, Amina. Aidha, tunamuomba Mwenyezi Mungu awajalie uponyaji wa haraka Watanzania wenzetu waliojeruhiwa ili waweze kurejea katika shughuli zao za kila siku za ujenzi wa Taifa.

## MAJUKUMU YA WIZARA

11. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mujibu wa Hati Idhini ya Rais (Presidential Instrument) iliyotolewa kupitia Tangazo la Serikali Na. 685 la tarehe 19 Desemba 2025, Wizara imekabidhiwa majukumu yafuatayo: -

i) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 (Toleo la mwaka 2023);

ii) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000;

iii) Kusimamia utawala wa ardhi;

iv) Kusimamia upangaji na uendelezaji wa miji na vijiji;

v) Kusimamia na kuwezesha upimaji wa ardhi na kutayarisha ramani;

vi) Kumilikisha ardhi na kuwezesha utoaji wa Hati za Hakimiliki ya Kimila;

vii) Kusajili Hatimiliki za Ardhi, Miamala na Nyaraka za Kisheria;

viii) Kusimamia uthamini wa mali;

ix) Kuhamasisha na kuwezesha ujenzi wa nyumba bora;

x) Kusimamia Uendelezaji Milki;

xi) Kusimamia utunzaji wa kumbukumbu za ardhi;

xii) Kusimamia ukusanyaji wa maduhuli yatokanayo na huduma za Sekta ya Ardhi;

xiii) Kuwezesha uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi na kufuatilia utekelezaji wake;

xiv) Kusimamia taasisi zilizo chini ya Wizara; na

xv) Kusimamia maslahi, utendaji kazi na maendeleo ya watumishi wa Wizara.

12. ***Mheshimiwa Spika,*** ardhi ni rasilimali muhimu inayotoa fursa kwa ajili ya maendeleo ya sekta mbalimbali na shughuli nyingine za kiuchumi na kijamii. Hivyo, sekta ya ardhi imeendelea kuwa sekta wezeshi kwa uwekezaji na uzalishaji katika sekta za viwanda, mifugo, kilimo, madini, ujenzi, uvuvi, maliasili, nishati na miundombinu na hivyo kuchangia katika kuongeza ajira kwa wananchi, pato la mwananchi mmoja mmoja, mapato ya Serikali na kukuza Pato la Taifa.

13. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/27 Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imepanga kutekeleza vipaumbele nane (**8**) kama ifuatavyo: -

i) Kuongeza kasi ya upangaji, upimaji, umilikishaji na usajili wa ardhi mijini, vijijini na maeneo ya kimkakati;

ii) Kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji;

iii) Kuimarisha mifumo ya TEHAMA katika utunzaji wa kumbukumbu, utoaji wa huduma, ukusanyaji wa maduhuli na upatikanaji wa taarifa za ardhi na uthamini;

iv) Kuimarisha mifumo ya utatuzi wa migogoro ya ardhi kwenye Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya;

v) Kuhakikisha uwepo wa nyumba bora, ukuaji wa sekta ya milki na maendeleo ya makazi kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii;

vi) Kuimarisha mipaka ya Kimataifa na kuendeleza miji ya mipakani;

vii) Kuimarisha upatikanaji wa ramani ili kuwezesha uandaaji wa mipango ya Kitaifa na matumizi mengine; na

viii) Kuimarisha mifumo ya usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa vipaumbele.

14. ***Mheshimiwa Spika,*** vipaumbele vilivyobainishwa vitawezesha kufikia malengo ya sekta yaliyoainishwa katika Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka, 1995 (Toleo la 2023); Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya Mwaka 2000; Dira 2050; Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025; Hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati akizindua Bunge la 13 mwezi Novemba 2025; Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2026/27-2030/31); Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030; na Mpango

Mkakati wa Wizara wa Miaka Mitano (2026/27-2030/31).

15. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya maelezo hayo ya utangulizi, majukumu na vipaumbele vya Wizara, naomba nitoe ufafanuzi kuhusu Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu **48**) pamoja na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu **03**) kwa mwaka 2025/26 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2026/27. Aidha, takwimu za utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2025/26 zilizopo katika hotuba hii zinaishia tarehe 15 Mei, 2026.

## MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2025/26 NA MALENGO YA MWAKA 2026/27

16. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imetekeleza majukumu yake kupitia Fungu **48** -Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Fungu **03** -Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi.

### Mapato na Matumizi ya Fedha (Fungu 48)

#### *Mapato*

17. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kukusanya shilingi bilioni **290** kutokana na vyanzo vya mapato ya

kodi ya pango la ardhi, ada na tozo mbalimbali za sekta ya ardhi. Hadi tarehe 15 Mei 2026, Wizara imekusanya shilingi bilioni **191.90** sawa na asilimia **66.17** ya lengo.

18. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/27, Wizara imepanga kukusanya shilingi bilioni **300** kutokana na kodi ya pango la ardhi, ada na tozo mbalimbali zinazohusiana na sekta ya ardhi. Lengo hilo litafikiwa kwa kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwemo kuendelea kusambaza miundombinu na mifumo ya TEHAMA katika Ofisi za Ardhi za Mikoa na Halmashauri ili kurahisisha utoaji wa huduma za ardhi; kuendelea kushirikiana na OWM-TAMISEMI kufuatilia halmashauri ambazo hazijakamilisha utekelezaji wa miradi ya KKK; kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kulipa kodi ya pango la ardhi kwa wakati; kuchukua hatua za kisheria kwa wadaiwa sugu ikiwemo kuwafikisha mahakamani na kuwasilisha taarifa zao kwa Kampuni ya Taarifa za Mikopo (Credit Information Reference Bureau-CIRB); kuendelea kubuni miradi ili kupata fedha kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za sekta na kuomba vibali vya ajira mpya ili kukidhi mahitaji ya rasilimaliwatu; kuendelea kuunganisha namba za simu za wamiliki wote wa ardhi ili waweze kupata jumbe fupi za kuwakumbusha kulipa kodi ya pango la ardhi kwa wakati; na

kuhakikisha viwanja vyote vilivyopimwa vinamilikishwa kwa wahusika. Wizara kwa kushirikiana na mamlaka nyingine inaendelea kutafuta njia bora ya ukusanyaji wa kodi ya pango la ardhi kupitia huduma mbalimbali zinazotolewa na taasisi hizo.

***Matumizi***

19. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Wizara iliidhinishiwa shilingi bilioni **153.44** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni **53.82** zilikuwa kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi, shilingi bilioni **37.56** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na shilingi bilioni **62.06** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo shilingi bilioni **5.73** ni Fedha za Maendeleo za Ndani na shilingi bilioni **56.33** ni Fedha za Maendeleo za Nje. Aidha, Wizara iliongezewa bajeti ya shilingi bilioni **64.24** ambapo shilingi bilioni **60.94** zilitumika kwa ajili kulipa madeni na shilingi bilioni **3.30** zilitumika kutetea maombi ya Eneo la Nyongeza Nje ya Ukanda wa Kiuchumi Baharini (Extended Continental Shelf) yaliyowasilishwa Umoja wa Mataifa, na hivyo kufanya Bajeti ya Maendeleo kuongezeka hadi shilingi bilioni **126.29** na Bajeti ya Wizara kufikia jumla ya shilingi bilioni **217.68**. Hadi tarehe 15 Mei 2026, Wizara imepokea shilingi bilioni **141.09**

kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo sawa na asilimia **64.82** ya bajeti. Kati ya fedha zilizopokelewa, shilingi bilioni **43.85** ni mishahara; shilingi bilioni **31.51** ni Matumizi Mengineyo na shilingi bilioni **65.74** ni kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha zilizopokelewa, shilingi bilioni **137.55** sawa na asilimia **95.51** zimetumika; ambapo shilingi bilioni **43.84** zilitumika kulipa mishahara ya watumishi, shilingi bilioni **29.82** zilitumika kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na shilingi bilioni **63.89** zilitumika kutekeleza miradi ya maendeleo (**Jedwali Na. 1**).

**Mapato na Matumizi ya Fedha: Fungu 03**

***Mapato***

20. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ilipanga kukusanya shilingi milioni **18** kupitia kodi ya pango la nyumba zilizopo mkoani Tabora. Hadi tarehe 15 Mei 2026, Tume imekusanya shilingi milioni **16.05** sawa na asilimia **89.17** ya lengo. Vilevile, Tume ilipanga kupokea michango ya shilingi bilioni **1** kutoka kwa wadau wa kimkakati. Hadi tarehe 15 Mei 2026, shilingi milioni **417.79** zilipokelewa sawa na asilimia **41.78** ya lengo. Kwa mwaka 2026/27, Tume imepanga kukusanya shilingi milioni **18**

kutokana na kodi ya pango la nyumba zilizopo mkoani Tabora. Aidha, juhudi za kuhamasisha wadau wa kimkakati kuchangia shilingi milioni **500** kwa ajili ya kugharamia shughuli za upangaji wa matumizi ya ardhi nchini zinaendelea.

***Matumizi***

21. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2025/26, Tume iliidhinishiwa shilingi bilioni **10.71**. Aidha, wakati wa utekelezaji wa bajeti, Tume iliongezewa shilingi bilioni **2** kwa ajili ya kugharamia Mradi wa Upangaji wa Matumizi ya Ardhi, hivyo jumla ya bajeti kuwa shilingi bilioni **12.71**. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni **4.71** ni Mishahara ya Watumishi, shilingi bilioni **3.48** ni Matumizi Mengineyo na shilingi bilioni **4.52** kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Upangaji wa Matumizi ya Ardhi. Hadi tarehe 15 Mei 2026, Tume imepokea shilingi bilioni **10.33** sawa na asilimia **81.27** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni **3.58** ni mishahara ya watumishi (PE), shilingi bilioni **2.23** ni Matumizi Mengineyo (OC) na shilingi bilioni **4.52** ni fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Upangaji wa Matumizi ya Ardhi. Aidha, kati ya fedha zote zilizopokelewa, jumla ya shilingi bilioni **10.24** sawa na asilimia **99.13** zimetumika. Kati ya fedha hizo zilizotumika, shilingi bilioni **3.58**

zilitumika kulipa mishahara ya watumishi, shilingi bilioni **2.23** zilitumika kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na shilingi bilioni **4.43** zilitumika kutekeleza Mradi wa Upangaji wa Matumizi ya Ardhi (**Jedwali Na. 2)**.

## UTAWALA WA ARDHI

22. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutoa huduma za ardhi kwa kushughulikia na kusimamia uandaaji na usajili wa Hatimiliki za ardhi, usimamizi wa masharti ya umiliki, ugawaji wa ardhi, utatuzi wa migogoro ya ardhi, usimamizi wa ardhi ya uwekezaji, uhuishaji wa kumbukumbu za ardhi na uthamini wa mali. Huduma hizi zimewezesha kuboresha taratibu za usimamizi wa ardhi na kuhakikisha wananchi wanakuwa na milki salama za ardhi zinazowawezesha kutumia milki hizo kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

### Uandaaji na Usajili wa Hati na Nyaraka za Kisheria

23. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kuandaa na kusajili Hatimiliki **500,000**, Hati za Hakimiliki ya Kimila **520,000**, Hati za Sehemu ya Jengo **1,000**, Vyeti vya Ardhi ya Kijiji **100** na Miamala ya Hatimiliki na Nyaraka za Kisheria **100,000**. Hadi tarehe 15 Mei 2026, Wizara imeandaa na

kusajili Hatimiliki **107,683** sawa na asilimia **21.54** ya lengo; Hati za Hakimiliki ya Kimila **99,762** sawa na asilimia **19.19** ya lengo; Vyeti vya Ardhi ya Kijiji **148** sawa na asilimia **148** ya lengo; na Hati za Sehemu ya Jengo **914** sawa na asilimia **91.4** ya lengo. Aidha, jumla ya Miamala ya Hatimiliki na Nyaraka za Kisheria **137,681** zimesajiliwa sawa na asilimia **137.68** ya lengo ambapo Miamala ya Hatimiliki ni **76,918** na Nyaraka za Kisheria ni **60,763** **(Jedwali Na. 3)**.



*Mhe. Dkt. Leonard Akwilapo Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi akikabidhi Hatimiliki kwa mwananchi wakati wa Kliniki Maalum ya Samia Ardhi Kliniki*



*Mhe. Kaspar Mmuya Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi akimkabidhi mwananchi Hati ya Hakimiliki ya Kimila Wilayani Ukerewe, mkoani Mwanza*

24. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2026/27, Wizara imepanga kuandaa na kusajili Hatimiliki **200,000**, Hati za Hakimiliki ya Kimila **300,000**, Vyeti vya Ardhi ya Kijiji **60**, Hati za Sehemu ya Jengo **1,000** na Miamala ya Hatimiliki na Nyaraka za Kisheria **100,000**. Ili kufikia lengo la utoaji wa Hatimiliki katika mwaka 2026/27, Wizara itaendelea kusambaza Mfumo wa e-Ardhi katika halmashauri zote nchini ili kurahisisha na kuongeza kasi ya umilikishaji ardhi, kuendelea kuhimiza wananchi

kuchangia gharama za urasimishaji na umilikishaji ardhi, kuziwezesha halmashauri kutekeleza Programu za Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi na kuendelea na Kliniki za Ardhi ili kusogeza huduma karibu zaidi na wananchi. **Natoa wito kwa wananchi kuhakikisha wanamiliki ardhi zao kisheria ili kuepuka migogoro na kuwawezesha kutumia ardhi kama mtaji wa kujiletea maendeleo.**

**Usimamizi wa masharti ya umiliki**

25. ***Mheshimiwa Spika***, sheria za ardhi zinamtaka kila mmiliki kuendeleza ardhi aliyomilikishwa kwa mujibu wa masharti yaliyoainishwa katika nyaraka za umiliki ikiwa ni pamoja na kulipa kodi ya pango la ardhi. Katika mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kufanya uhakiki na ukaguzi wa viwanja na mashamba **1,000** ili kubaini wamiliki wasiozingatia masharti ya umiliki na kuwachukulia hatua za kisheria. Hadi tarehe 15 Mei 2026, jumla ya viwanja na mashamba **2,503** yalikaguliwa. Ukaguzi huo ulibaini kuwa wamiliki **1,571** wa viwanja na mashamba walizingatia masharti ya umiliki na wamiliki **932** wa viwanja na mashamba walikiuka masharti ya umiliki. Wizara imeendelea kuchukua hatua za kisheria kwa wamiliki waliokiuka masharti ya umiliki ambapo milki za mashamba na viwanja **15** zimefutwa na hatua za kisheria zinaendelea

kuchukuliwa kwa wamiliki **917**. Katika mwaka 2026/27, Wizara itaendelea kufanya uhakiki na ukaguzi wa viwanja na mashamba **1,000** ili kubaini hali ya uendelezaji na kuchukua hatua stahiki. **Natoa rai kwa wamiliki wa ardhi kuendeleza milki zao kwa mujibu wa masharti ya umiliki ili kuepuka Serikali kubatilisha milki hizo.**

**Usimamizi wa Ardhi ya Uwekezaji**

26. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inasimamia uidhinishaji wa maombi ya ardhi kwa ajili ya uwekezaji. Ardhi ya uwekezaji hutambuliwa, hutangazwa na kumilikishwa kwa Mamlaka ya Uwekezaji na Maeneo Maalum ya Kiuchumi Tanzania (TISEZA) ambayo hutoa Hatimiliki Isiyo Asili (Derivative Right) kwa wawekezaji. Pamoja na jitihada binafsi zinazofanywa na wawekezaji ili kupata ardhi, Wizara imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ili kuhakikisha kuwa kuna ardhi kwa ajili ya uwekezaji. Mikakati hiyo ni pamoja na kutenga ardhi kwa ajili ya uwekezaji kupitia Mipango Kabambe inayoandaliwa, Mradi wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi na ardhi ya mashamba yaliyobatilishwa. Jukumu hilo linatekelezwa na Kamati ya Taifa ya Ugawaji Ardhi iliyo chini ya Wizara ambayo huchambua, kujadili na kuidhinisha maombi ya ardhi kwa ajili ya uwekezaji. Katika mwaka 2025/26, Wizara

ilipanga kugawa hekta **5,000** kwa wawekezaji. Hadi tarehe 15 Mei 2026, Wizara kupitia Kamati ya Kitaifa ya Ugawaji Ardhi imepokea na kuidhinisha maombi **333** ya ardhi ya uwekezaji yenye ukubwa wa hekta **45,371.24.** Kati ya maombi yaliiyoidhinishwa, maombi **81** yenye ukubwa wa hekta **5,802.14** ni ya wawekezaji wa ndani na maombi **252** yenye ukubwa wa hekta **39,569.10** ni ya wawekezaji kutoka nje. Katika mwaka 2026/27, Wizara itatenga na kugawa ardhi yenye ukubwa wa hekta **5,000** kwa ajili ya uwekezaji.




*Kamati ya Kitaifa ya Ugawaji Ardhi ikikagua shamba la mwekezaji jijini Arusha*

27. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kufikia azma ya Serikali ya kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji nchini, Wizara imeendelea kuweka mikakati ya kuimarisha utoaji wa huduma kwenye Mamlaka ya Uwekezaji na Maeneo Maalum ya Kiuchumi Tanzania (TISEZA) kwa kuanzisha ofisi maalum ya ardhi kwa ajili ya kushughulikia masuala ya uwekezaji. Aidha, Wizara imeendelea kuimarisha utoaji wa huduma za ardhi kwenye mikoa ya Dodoma, Dar es Salaam na Mwanza ambayo ina mahitaji makubwa ya huduma kwa kuanzisha ofisi mpya za ardhi kwenye mikoa hiyo. Hivyo, mikoa hiyo imekuwa na Makamishna wa Ardhi Wasaidizi wawili hatua ambayo itaongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa kuwafikia wananchi karibu zaidi na maeneo yao. **Napenda kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maono na dhamira yake ya kuhakikisha wawekezaji na wananchi wanapata huduma bora za ardhi kwa ajili ya kujiletea maendeleo ya kiuchumi na kijamii.**

**Uhuishaji wa Kumbukumbu za Ardhi**

28. ***Mheshimiwa Spika***, katika kukabiliana na changamoto za upatikanaji wa taarifa sahihi za wamiliki wa ardhi, Wizara inaendelea kuhuisha kumbukumbu za ardhi na kuziingiza katika

Mifumo ya TEHAMA ili kuwezesha utoaji wa huduma kwa urahisi, usahihi na kwa muda mfupi. Uhuishaji huo unahusisha ubadilishaji wa nyaraka za hatimiliki na majalada kutoka analojia kwenda mfumo wa kidijiti, uhakiki na uhuishaji wa taarifa za wamiliki pamoja na kubainisha ukubwa wa viwanja, matumizi na mahali vilipo. Katika mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kuhuisha kumbukumbu za wamiliki wa ardhi **500,000**. Hadi tarehe 15 Mei 2026, kumbukumbu za ardhi **146,345** zimehuishwa. Katika mwaka 2026/27, Wizara itaendelea kuhuisha kumbukumbu za wamiliki wa ardhi **500,000** na kuziingiza katika Mfumo wa e-Ardhi.



*Watumishi wakiendelea na kazi ya kubadilisha taarifa za ardhi kutoka nakala ngumu kwenda nakala tete (Data Conversion)*

## Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi Kiutawala

29. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea na utatuzi wa migogoro ya ardhi kiutawala kwa kutumia njia mbalimbali ikiwemo uendeshaji wa Kliniki za Ardhi kwenye mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, madawati ya kushughulikia kero na malalamiko, timu na kamati maalum za wataalam wa Serikali na ziara za viongozi wa Wizara katika maeneo mbalimbali nchini. Utatuzi huo unahusisha changamoto za ardhi zinazotokana na masuala ya fidia; milki pandikizi; mwingiliano wa mipaka ya vijiji, viwanja au mashamba; uvamizi wa maeneo ya umma na binafsi; udanganyifu na utapeli kwa kutumia nyaraka za kughushi; madai ya mali za urithi au wanandoa; na changamoto zinazotokana na zoezi la urasimishaji makazi na upimaji shirikishi wa ardhi. Kadhalika, yapo malalamiko yanayotokana na wananchi kutoridhika na uamuzi wa vyombo vinavyotoa haki kisheria.



*Mhe. Dkt. Leonard Akwilapo, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi akizungumza na wananchi wa Mahomanyika Dodoma wakati wa kushughulikia mgogoro wa ardhi*

30. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na kuwepo kwa migogoro ya ardhi inayoendelea kujitokeza katika maeneo mbalimbali nchini, **Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa**

**Tanzania Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba** alielekeza Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuandaa mkakati wa kupata ufumbuzi wa kudumu wa migogoro hiyo. Kufuatia maelekezo hayo, Serikali imeandaa na kuanza utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Kudhibiti Migogoro ya Ardhi Nchini. Mkakati huo unahusisha wadau na makundi yote muhimu hususan wakulima, wafugaji, wawekezaji na mamlaka za hifadhi ili kuhakikisha changamoto ya migogoro ya ardhi inapatiwa ufumbuzi wa kudumu. **Napenda kutumia fursa hii kumshukuru tena Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa dhamira yake ya dhati ya kuhakikisha migogoro ya ardhi inadhibitiwa hivyo kuwawezesha watumiaji wa ardhi kufanya kazi zao kwa amani na utulivu.**

31. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kushughulikia migogoro ya ardhi **3,000**. Hadi tarehe 15 Mei 2026, jumla ya migogoro ya ardhi **5,573** imetatuliwa ambapo kati ya hiyo, migogoro **3,183** imetatuliwa kupitia Kliniki za Ardhi na **2,390** kupitia utaratibu wa kawaida wa kiutawala (**Jedwali Na. 4**). Katika mwaka 2026/27, Wizara imepanga kushughulikia migogoro **4,000** kiutawala. **Natoa rai kwa viongozi, watumishi na wananchi kwa ujumla kuzingatia**

**sheria za ardhi, kanuni na miongozo ili kuepuka kuanzisha migogoro mipya**.

**Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi katika Vijiji/ Mitaa 975**

32. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kuendelea kuratibu ukamilishaji wa kazi zilizobaki za utekelezaji wa uamuzi wa Baraza la Mawaziri kuhusu Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi katika Vijiji/Mitaa **975**. Uamuzi umeendelea kutekelezwa ikiwemo kurejesha ardhi kwa wananchi ambapo ekari milioni **3.13** zimerejeshwa na shilingi bilioni **95.27** zimelipwa kwa wananchi waliostahili kulipwa fidia katika maeneo **14 (Jedwali Na. 5)**. Kazi hiyo imefanywa na timu ya wataalam kutoka taasisi na wizara za kisekta.

33. ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia tathmini iliyofanyika, mpango kazi kwa ajili ya kukamilisha kazi zilizobaki umeandaliwa. Hivyo, naomba kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi na Wizara za Kisekta, itaendelea kuratibu ukamilishaji wa kazi hizo. Utekelezaji husika utahusisha vijiji **349** na mitaa **11** ambayo sehemu ya utekelezaji wa maamuzi umeanza kufanyiwa kazi, pamoja na vijiji **166** ambavyo utekelezaji wake utafanyika katika mwaka 2026/27.

## Uthamini wa Mali

34. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara yangu pia inasimamia uthamini wa mali zinazohamishika na zisizohamishika, uidhinishaji wa taarifa za uthamini na uandaaji wa viwango vya bei ya soko la ardhi, mazao na majengo. Viwango vya bei ya soko ndivyo hutumika kufanya uthamini ili kuwezesha ulipaji wa fidia, utozaji wa ushuru wa Serikali unaotokana na mauzo au uhamisho wa umiliki wa mali, utozaji wa malipo ya awali (premium) wakati wa kutoa milki, mizania ya hesabu, kuweka mali rehani, mirathi, kinga ya bima na utozaji kodi ya pango la ardhi.

35. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kuidhinisha taarifa za uthamini **54,000** ambapo kati ya hizo, taarifa za uthamini wa kawaida ni **20,000** na majedwali ya fidia yenye wafidiwa **34,000.** Aidha, Wizara ilipanga kushughulikia malalamiko **100** yatokanayo na uthamini, kukamilisha uandaaji wa vitalu vya thamani ya ardhi katika mikoa saba (**7**) na kuendelea na zoezi la kuhuisha viwango vya thamani ya ardhi katika mikoa **26**. Hadi tarehe 15 Mei 2026, Wizara imeidhinisha taarifa za uthamini **57,293** sawa na asilimia **106.10** ya lengo ambapo kati ya hizo, taarifa za uthamini wa kawaida ni **27,211** na majedwali ya fidia yenye wafidiwa **30,082**.

Aidha, malalamiko ya uthamini **99** yalipokelewa na kushughulikiwa kiutawala. Vilevile, zoezi la kuhuisha viwango vya thamani ya ardhi na mazao limefanyika katika mikoa **26** nchini na uhuishaji wa viwango vya thamani ya majengo umefanyika katika mikoa ya Dar es Salaam na Dodoma.

36. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara pia imeendelea kushiriki katika kufanya uthamini wa mali katika maeneo yanayotwaliwa ili kupisha miradi mikubwa ya kimkakati inayotekelezwa na Serikali. Kazi zilizofanyika ni pamoja na uthamini wa mali za wananchi wanaotakiwa kupisha miradi ya reli ya kisasa–SGR kipande cha Tabora Kigoma na Tabora– Shinyanga; utafiti wa mafuta na gesi katika kitalu cha Lindi– Mtwara; maeneo ya uwekezaji; na miradi ya maji, barabara na umeme. Katika mwaka 2026/27, Wizara imepanga kuidhinisha taarifa za uthamini **50,000** ambapo kati ya hizo, taarifa za uthamini wa kawaida ni **20,000** na taarifa za fidia zenye wafidiwa ni **30,000**; kushughulikia malalamiko **100** yatokanayo na uthamini; na kuhuisha kanzidata ya viwango vya thamani ya ardhi, mazao na majengo katika mikoa **26**.



*Wataalamu wakiwa katika zoezi la uthamini katika eneo la Mradi wa Reli ya SGR Tabora-Kigoma kipande cha sita mkoani Kigoma*



*Elimu ya uthamini wa fidia ikitolewa kwa wananchi wanaopisha Mradi wa Ujenzi wa Reli ya SGR Tabora-Kigoma Kipande cha sita*

## MABARAZA YA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA

37. ***Mheshimiwa Spika,*** mojawapo ya jukumu la Wizara ni kuanzisha na kusimamia Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya ambayo yanasikiliza na kuamua migogoro ya ardhi kisheria. Katika kutekeleza jukumu hilo, Wizara imeendelea kuanzisha Mabaraza katika wilaya mbalimbali nchini ambayo yamekuwa yakisikiliza na kuamua mashauri ya ardhi. Katika mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kuanzisha Mabaraza mapya **24** na kushughulikia mashauri **16,000**. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi tarehe 15 Mei 2026, Wizara imeanzisha Mabaraza mapya sita (**6**) na hivyo kuwa na jumla ya Mabaraza **121** yanayofanya kazi. Aidha, mashauri **23,426** yamesikilizwa ambapo kati ya hayo, mashauri **12,644** yameshughulikiwa na kutolewa uamuzi na mashauri **10,782** yanaendelea kushughulikiwa. Katika mwaka 2026/27, Wizara itaanzisha Mabaraza mapya **18** ili kufikia lengo la kuwa na Mabaraza ya Ardhi na Nyumba katika wilaya zote **139** zilizopo nchini. Aidha, Wizara itaendelea kushughulikia mashauri **10,782** yaliyobaki na yatakayofunguliwa. **Natoa wito kwa wenyeviti wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya kuzingatia weledi, uadilifu na misingi ya utoaji haki katika kuamua**

**mashauri ya ardhi ili kujenga imani kwa wananchi wanaopata huduma katika Mabaraza yetu.**

**HUDUMA ZA TEHAMA**

38. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutumia mifumo ya TEHAMA katika kuongeza ufanisi wa utendaji kazi na utoaji huduma kwa wananchi, kuongeza uwazi na uwajibikaji na kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali. Katika mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kusimika miundombinu ya TEHAMA katika ofisi za ardhi za mikoa na halmashauri zote nchini, kusambaza Mfumo wa e-Ardhi, kutoa elimu na kuwajengea uwezo watumiaji. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Wizara imesambaza vifaa vya TEHAMA vyenye thamani ya shilingi bilioni **5.20** katika mikoa na halmashauri zote nchini. Aidha, huduma za uthamini na usajili wa nyaraka zinatolewa kupitia Mfumo wa e-Ardhi nchi nzima na huduma za utawala wa ardhi zinatolewa kupitia mfumo huo katika mikoa mitano (**5**) ya Arusha, Dodoma, Mbeya, Tanga na Mwanza pamoja na baadhi ya halmashauri za mikoa ya Shinyanga, Kigoma, Tabora, Mtwara, Pwani na Ruvuma. Katika mwaka 2026/27, Wizara itaendelea na juhudi za kuhakikisha huduma zote zinapatikana kupitia mfumo huo katika ofisi zote za ardhi za mikoa na halmashauri

nchini, sambamba na kusafisha na kubadili taarifa za kijiografia na majalada ya umiliki wa ardhi kutoka analojia kwenda kidijiti, ambayo ni hatua muhimu ya usambazaji wa mfumo huu.




*Mhe. Dkt. Leonard Akwilapo, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (kushoto) akimkabidhi vifaa vya TEHAMA Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Mtwara Bw. Fredrick Mrema (katikati). Kulia ni Katibu Mkuu Mhandisi Anthony Sanga*

39. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imerahisisha huduma za malipo ikiwa ni pamoja na wananchi kutumiwa au kutengeneza ankara zao bila kulazimika kufika kwenye Ofisi za Ardhi,

kulipia kodi ya pango la ardhi wakati wowote na mahali popote kupitia simu, mawakala au benki ambapo kwa sasa namba ya malipo ni ya kudumu. Hadi tarehe 15 Mei 2026, wananchi **127,449** wamejengewa uwezo, kujisajili na kuhudumiwa kupitia mfumo. **Natoa wito kwa wananchi kuendelea kufuatilia matangazo yanayotolewa katika vyombo mbalimbali vya habari, mitandao ya kijamii na tovuti ya Wizara ili kujifunza kuhusu huduma za sekta ya ardhi zinazotolewa kupitia Mfumo wa e-Ardhi**.

## UPIMAJI ARDHI NA UTAYARISHAJI WA RAMANI

40. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza jukumu la kusimamia na kuratibu shughuli zote za uwekaji wa alama za msingi; upimaji ardhi nchi kavu na ndani ya maji kwa ajili ya shughuli za haidrografia; na utayarishaji wa ramani za msingi, ramani za mipaka ya kiutawala na ramani za matumizi mbalimbali kwa ajili ya *utekelezaji* wa mipango ya Serikali na shughuli za maendeleo. Pia, Wizara imeendelea kutoa miongozo ya upimaji ardhi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali katika utekelezaji wa majukumu hayo.

## Uwekaji Alama za Msingi za Upimaji Ardhi

41. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha kuwa kazi za Upimaji nchini zinatekelezwa kwa ufanisi, Wizara imeendelea kuongeza Alama za Msingi za Upimaji (Control Points) na kuanza usimikaji wa alama za msingi zinazoendana na teknolojia ambazo ni Vituo vya Kielektroniki vya Upimaji (Continuously Operating Reference Stations- CORS) ambavyo ni miongoni mwa miundombinu muhimu katika kurahisisha kazi za upimaji kwa kupunguza muda na gharama za upimaji.

42. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kuweka Alama mpya za Msingi za Upimaji **438** katika halmashauri mbalimbali nchini pamoja na kukamilisha ujenzi na usimikaji wa Vituo vya Kielektroniki vya Upimaji **22** katika mikoa **20** ya Dodoma, Iringa, Pwani, Kagera, Njombe, Mara, Dar es Salaam, Manyara, Rukwa, Arusha, Mtwara, Ruvuma, Geita, Katavi, Mwanza, Kigoma, Shinyanga, Singida, Morogoro na Tanga. Hadi tarehe 15 Mei 2026, Alama za Msingi za Upimaji **55** zimewekwa katika mikoa ya Kilimanjaro (**15**) na Mbeya (**40**). Aidha, ujenzi na usimikaji wa Vituo vya Kielektroniki vya Upimaji **22** umekamilika na vituo vitatu (**3**) vya Kielektroniki vilivyopo mikoa ya Dar es Salaam, Kilimanjaro na Tabora vimehuishwa. Vilevile, vituo vyote vimeanza kutumika katika

shughuli mbalimbali za upimaji. Katika mwaka 2026/27, Wizara itaongeza Alama za Msingi za Upimaji **438** pamoja na kuwezesha matengenezo ya vituo vya Kielektroniki vya Upimaji vilivyojengwa maeneo mbalimbali nchini.

**Upigaji Picha za Anga**

43. ***Mheshimiwa Spika,*** picha za anga ni muhimu kwa ajili ya kupata taarifa za msingi zinazotumika kuandaa ramani za msingi na ramani za matumizi maalum kama vile kupata taarifa za sura ya nchi, kupanga na kutathmini maendelezo ya miji. Katika mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kupiga picha za anga katika eneo lenye ukubwa wa kilomita za mraba **1,000** na kuhuisha ramani za msingi pamoja na ramani nyingine katika wilaya mbalimbali. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi tarehe 15 Mei 2026, Wizara imepiga picha za anga katika eneo lenye ukubwa wa kilomita za mraba **204.09** katika mikoa ya Dodoma (**44.89**), Geita (**158.3**) na Dar es Salaam (**0.9**). Aidha, ramani za mipaka ya kiutawala katika halmashauri za wilaya tano (**5**) zimeandaliwa ambazo ni Kongwa, Kondoa, Ushetu, Kaliua na Singida. Katika mwaka 2026/27, Wizara itaendelea kupiga picha za anga katika eneo lenye ukubwa wa kilomita za mraba **1,000** na kuhuisha ramani za msingi pamoja na ramani nyingine katika wilaya mbalimbali nchini.

**Tafsiri ya Matangazo ya Serikali kuhusu Maeneo ya Utawala (GN)**

44. ***Mheshimiwa Spika,*** tafsiri ya Matangazo ya Serikali (GN) kuhusu maeneo ya utawala na hifadhi ni suala muhimu katika kutambua maeneo na kuwezesha utatuzi wa migogoro ya mipaka ya ardhi nchini. Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta na Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI imeendelea kutafsiri Matangazo ya Serikali (GN) ya maeneo ya utawala na hifadhi. Tafsiri hizo zinawezesha kutatua migogoro ya mipaka ya vijiji, wilaya, mikoa na hifadhi. Katika mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kutafsiri Matangazo ya Serikali (GN) **10** ili kuwezesha utatuzi wa migogoro ya mipaka ya ardhi. Hadi tarehe 15 Mei 2026, Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta imefanya tafsiri ya matangazo ya maeneo ya hifadhi tatu (**3**) za Burigi Chato, Selous na Udzungwa pamoja na mipaka ya kiutawala minne (**4**) katika wilaya za Kongwa, Chemba, Kondoa na Singida. Katika mwaka 2026/27, Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta na Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI imepanga kutafsiri Matangazo ya Serikali (GN) **10** ili kuwezesha utatuzi wa migogoro ya mipaka ya ardhi.

## Upimaji wa Viwanja na Mashamba

45. ***Mheshimiwa Spika,*** upimaji wa ardhi huwezesha kuwa na mipaka iliyotambuliwa kisheria na hivyo kuongeza usalama wa milki, thamani ya ardhi na kuepusha migogoro inayohusiana na mipaka ya ardhi. Wizara imeendelea kuratibu na kusimamia upimaji wa viwanja na mashamba unaofanywa na mamlaka za upangaji na sekta binafsi. Katika mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kuratibu upimaji na uidhinishaji wa viwanja **500,000** na mashamba ***500***. Hadi tarehe 15 Mei 2026, viwanja **193,317** na mashamba **515** yamepimwa na kuidhinishwa sawa na asilimia **38.66** na **103** mtawalia (**Jedwali Na. 6**). Katika mwaka 2026/27, Wizara imepanga kupima na kuidhinisha viwanja **500,000** na mashamba **500**.



*Wataalam wa sekta ya ardhi wakiwa kwenye zoezi la upimaji wa mashamba*

## Upimaji wa Mipaka ya Vijiji

46. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina jukumu la kuratibu na kupima mipaka ya vijiji kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kwa lengo la kuimarisha usimamizi wa mipaka ya kiutawala. Katika mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kuhakiki na kupima mipaka ya vijiji **100**. Hadi tarehe 15 Mei 2026, mipaka ya vijiji **54** imehakikiwa na kuhuishwa na vijiji **189** vimepimwa na hivyo kufanya vijiji vilivyopimwa kufikia **11,996** kati ya vijiji **12,333** vilivyopo nchini (**Jedwali Na. 7**). Katika mwaka 2026/27, Wizara itaendelea kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI na wadau wa maendeleo kuhakiki, kuhuisha na kupima mipaka ya vijiji **226** nchini. Katika kutekeleza jukumu hili, Wizara imeendelea kupokea malalamiko kutoka kwa wananchi dhidi ya Serikali za Vijiji kuhusu kuathiriwa haki zao za ardhi baada ya kubainishwa kwa mipaka ya vijiji. **Nitumie fursa hii kuzitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa kuheshimu haki za ardhi za wananchi ili kuondoa migogoro**.

## UPANGAJI MIJI NA MAENDELEO YA MAKAZI

47. ***Mheshimiwa Spika,*** usimamizi wa usanifu na upangaji wa miji ni miongoni mwa majukumu yanayotekelezwa na Wizara kwa mujibu wa Sheria ya Mipangomiji, Sura ya 355. Majukumu haya yanajumuisha uandaaji wa

Mipango ya Jumla (Mipango Kabambe), Mipangokina, utangazaji wa maeneo yaliyoiva kwa upangaji, maeneo maalum ya upangaji, udhibiti wa uendelezaji miji, urasimishaji makazi na usimamizi na uratibu wa uendelezaji nyumba.

## Utangazaji wa Maeneo ya Upangaji Miji

48. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina jukumu la kutangaza maeneo yaliyoiva kuendelezwa kimji kwa mujibu wa Sheria ya Mipangomiji, Sura ya 355. Baadhi ya vigezo vya kutangaza eneo kuendelezwa kimji ni pamoja na idadi ya watu wasiopungua **10,000**, uwepo wa huduma za msingi za kiuchumi na kijamii kama vile zahanati au kituo cha afya, shule ya msingi, maeneo ya wazi, soko na maduka yasiyopungua matano (**5**). Wizara hutangaza maeneo yenye sifa hizi baada ya kupokea mapendekezo kutoka kwenye Mamlaka za Upangaji. Maeneo hayo huandaliwa Mipangokina na Mamlaka za Upangaji kwa kushirikiana na wananchi na wadau mbalimbali.

49. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kuendelea kutangaza maeneo mapya ya upangaji miji na urasimishaji makazi ili kuendelea kusimamia uendelezaji na ukuaji endelevu wa miji nchini. Hadi tarehe 15 Mei 2026, Wizara ilipokea na kutangaza maeneo **42** kutoka katika Mamlaka za Upangaji **29**. Maeneo hayo

yamepandishwa hadhi kutoka vijiji na kuwa maeneo ya mipangomiji (**Jedwali Na. 8**). Katika mwaka 2026/27, Wizara itaendelea kushirikiana na Mamlaka za Upangaji kutambua, kupokea mapendekezo na kutangaza maeneo yaliyoiva kuendelezwa kimji.

**Uandaaji wa Mipango ya Jumla**

50. ***Mheshimiwa Spika,*** ukuaji na uendelezaji wa miji huongozwa na Mipango ya Jumla inayoainisha matumizi mbalimbali ya ardhi katika miji nchini. Katika mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kushirikiana na Halmashauri mbalimbali nchini kuratibu, kusimamia na kutoa ushauri wa kitaalam kwenye Mamlaka za Upangaji kuhusu uandaaji wa Mipango ya Jumla. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, maandalizi ya Mipango ya Jumla ya miji minne (**4**) ya Mkuranga, Kwala, Mafinga na Manispaa ya Kahama yanaendelea. Vilevile, ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mipango ya Jumla iliyoandaliwa umefanyika katika majiji ya Arusha, Dodoma, Tanga na Mbeya pamoja na Manispaa za Shinyanga na Morogoro. Ufuatiliaji huo umebaini kuwa Mipangokina inayoandaliwa inazingatia Mipango ya Jumla inayosimamia ukuaji wa miji hiyo. Aidha, Serikali kupitia Mradi wa *Tanzania Cities Transforming Infrastructure and Competitiveness* (TACTIC) ambao unasimamiwa na kuratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu -

TAMISEMI inaendelea na maandalizi ya awali ya kuandaa Mipango ya Jumla ya miji mingine **18** nchini **(Jedwali Na. 9)**.

51. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/27, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji itaendelea kufuatilia uandaaji na utekelezaji wa Mipango ya Jumla kwa mujibu wa sera, sheria, kanuni na miongozo iliyopo ili kuchochea maendeleo endelevu ya ukuaji wa miji nchini. **Natoa wito kwa Mamlaka za Upangaji nchini kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya uandaaji wa Mipango ya Jumla pamoja na kuhakikisha utekelezaji wa miradi inayopangwa inazingatia mipango hiyo.**

**Uandaaji wa Mipangokina**

52. ***Mheshimiwa Spika,*** Mipangokina (Michoro ya Mipangomiji) ni mipango inayoongoza matumizi ya ardhi katika kiunga cha mji kwa kusanifu matumizi mbalimbali yanayohitajika kuwezesha jamii kuishi, kufanya kazi na kufurahia mandhari ya eneo husika. Mipango hii hutafsiri Mipango ya Jumla ardhini na huandaliwa na Mamlaka za Upangaji kwa lengo la kuelekeza ukuaji na uboreshaji wa makazi, kuhifadhi mazingira, kuondoa ukinzani wa matumizi ya ardhi na kutoa uhakika wa upatikanaji wa maeneo yenye matumizi mbalimbali.

53. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kupokea, kukagua na kuidhinisha michoro ya mipangomiji **2,000** kutoka katika Mamlaka za Upangaji nchini. Hadi tarehe 15 Mei 2026, jumla ya michoro ya mipangomiji **3,695** sawa na asilimia **184.75** yenye jumla ya viwanja **315,287** imeidhinishwa (**Jedwali Na**. **10**). Katika mwaka 2026/27, Wizara itapokea, kukagua na kuidhinisha michoro ya mipangomiji **2,000** kutoka katika Mamlaka za Upangaji nchini.

**Urasimishaji Makazi**

54. ***Mheshimiwa Spika,*** urasimishaji makazi unahusisha kuboresha makazi yaliyoendelezwa bila kupangwa kwa kuyatambua, kuyapanga, kuyapima na kumilikisha ili kuimarisha upatikanaji wa huduma za jamii na miundombinu, kuongeza usalama wa milki na uhifadhi wa mazingira. Katika mwaka 2025/26, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji ilipanga kuendelea kuratibu urasimishaji makazi **200,000** katika halmashauri zote nchini. Hadi tarehe 15 Mei 2026, jumla ya makazi **149,784** sawa na asilimia **74.89** yamerasimishwa (**jedwali Na. 11).** Katika mwaka 2026/27, Wizara itaendelea kuratibu urasimishaji wa makazi **200,000**.

**Udhibiti wa Uendelezaji Miji**

55. ***Mheshimiwa Spika,*** udhibiti wa uendelezaji miji ni suala mtambuka linalotekelezwa na Wizara kwa kushirikisha Mamlaka za Upangaji na wadau wengine. Kutokana na ongezeko la watu, shughuli za kiuchumi na kukua kwa teknolojia, miji hubadilika na kuhitaji uratibu katika uendelezaji wake ikiwemo mabadiliko ya matumizi ya ardhi kwa lengo la kuongeza tija katika matumizi ya ardhi mijini ili kukuza uchumi na Pato la Taifa. Kwa muktadha huo, Wizara ina jukumu la kupokea, kukagua na kuidhinisha maombi ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi yanayowasilishwa kutoka kwenye Mamlaka za Upangaji.

56. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kukagua na kuidhinisha maombi **300** ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi kutoka kwenye Mamlaka za Upangaji nchini. Hadi tarehe 15 Mei 2026, Wizara ilipokea na kuidhinisha jumla ya maombi **730** ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi ambayo ni sawa na asilimia **236.67** ya lengo. Ongezeko hilo limetokana na kuboreshwa kwa huduma za sekta ya ardhi na miundombinu inayochochea mahitaji ya uwekezaji na biashara katika maeneo ya miji. Katika mwaka 2026/27, Wizara itaendelea kuratibu shughuli za udhibiti wa uendelezaji wa miji kwa kuidhinisha

maombi **300** ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi. **Natoa wito kwa Mamlaka za Upangaji kuzingatia sheria katika utoaji wa vibali vya uendelezaji ardhi (Planning Consent) kabla ya kutoa vibali vya ujenzi ili kuwaelekeza wamiliki wa ardhi namna ya kutumia ardhi zao kwa kuzingatia ukubwa wa eneo la kiwanja na matumizi yaliyokusudiwa. Aidha, ujenzi unaofanyika bila vibali udhibitiwe ili kuzuia ukuaji holela wa miji.**

**Uendelezaji Upya na Uboreshaji wa Maeneo Chakavu Mijini**

57. ***Mheshimiwa Spika,*** Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000 imehimiza uboreshaji wa makazi chakavu kwa kuweka miundombinu na huduma za jamii ili kuboresha mandhari ya miji na kuongeza fursa za kiuchumi na mchango wa maeneo hayo katika Pato la Taifa. Kwa kuzingatia takwa hilo la kisera, Wizara imeanza kutekeleza Programu Maalum ya Uendelezaji Upya wa Maeneo Chakavu (Land Re-adjustment Program) katika miji mbalimbali nchini. Jumla ya maeneo **111** yenye ukubwa wa hekta **24,309.3** yameainishwa katika halmashauri **35** zilizopo kwenye mikoa **25** (**Jedwali Na. 12**).

58. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/ 26, Wizara ilipanga kuratibu uendelezaji upya wa eneo la Makangira- Msasani katika Manispaa ya Kinondoni

lenye ukubwa wa hekta **17.20** kama eneo la mfano. Kazi ya kuendeleza eneo hilo imeanza kwa kuwashirikisha wananchi ambapo ukusanyaji wa taarifa na utambuzi wa milki za wakazi wa eneo hilo umefanyika. Taarifa hizo zitawezesha kufahamu hali halisi ya maisha ya wakazi wa eneo hilo, thamani ya rasilimali zilizopo, mahitaji na matamanio ya wananchi na namna ya kufanya mgawanyo wa milki zitakazoboreshwa katika eneo hilo. Katika mwaka 2026/27, Wizara itaanza upangaji na upimaji wa ardhi sambamba na kutafuta wawekezaji wenye sifa na uwezo wa kuendeleza eneo hilo.



*Zoezi la ukusanyaji wa taarifa na utambuzi wa milki za makazi kwa wananchi kwa ajili ya uboreshaji maeneo chakavu ya miji katika eneo la Makangira, Msasani wilaya ya Kinondoni Mkoa wa Dar es Salaam*

59. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imekamilisha rasimu ya mpango wa uendelezaji upya eneo la Sinza katika Manispaa ya Ubungo ambapo wananchi na wadau mbalimbali wanaendelea kutoa maoni. Mpango huu unalenga kuongeza thamani ya uwekezaji wenye tija katika kuboresha maisha ya wananchi na kuongeza Pato la Taifa kwa kusanifu matumizi mchanganyiko yatakayowezesha kuongeza viwango vya ujenzi wa eneo hilo kuanzia sakafu mbili (**2**) hadi **20** kulingana na uhimilivu wa uwezo wa ardhi. **Natoa wito kwa wananchi na sekta binafsi kuchangamkia fursa kwenye maeneo yote mawili na kushiriki kikamilifu katika kufanikisha utekelezaji wa mipango hiyo kwa manufaa endelevu ya wananchi na Taifa kwa ujumla. Aidha, Nitumie fursa hii kuwahakikishia wamiliki wa ardhi katika maeneo hayo kuwa hakuna ardhi itakayochukuliwa na Serikali katika utekelezaji wa mpango huu.**

**Usimamizi na Uratibu wa Uendelezaji Nyumba**

60. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza jukumu la kusimamia na kuratibu uendelezaji wa nyumba nchini zoezi ambalo hufanywa na taasisi za umma, sekta binafsi na Vyama vya Ushirika wa Nyumba. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali ikiwemo Benki Kuu ya Tanzania imeendelea kuweka mazingira wezeshi ya upatikanaji wa huduma za

uendelezaji nyumba nchini. Huduma hizo ni pamoja na: - upatikanaji wa mikopo ya masharti nafuu kwa ajili ya ujenzi wa nyumba, ubunifu wa nyumba za gharama nafuu na utoaji wa mikopo ya nyumba kwa watumishi wa Serikali.

**Mikopo ya Ujenzi wa Nyumba**

61. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ilianzisha Taasisi ya *Tanzania Mortgage Refinance Company* (TMRC) kwa ajili ya kuwezesha taasisi za fedha kutoa mikopo ya muda mrefu ya ujenzi wa nyumba kwa wananchi. Hadi tarehe 15 Mei 2026, jumla ya shilingi bilioni **720.81** zimetolewa kwa wananchi **5,802** kupitia taasisi za fedha **29** (**Jedwali Na. 13**).

62. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kutoa mikopo kwa watumishi wa Serikali **137** yenye thamani ya shilingi bilioni **2.60**. Hadi tarehe 15 Mei 2026, jumla ya shilingi bilioni **2.94** zimetolewa kwa watumishi **111** sawa na asilimia **81** ya lengo na hivyo kufanya jumla ya watumishi waliopata mikopo tangu kuanzishwa kwa mfuko huo kufikia **1,921** yenye thamani ya shilingi bilioni **12.34**. Katika mwaka wa fedha 2026/27, Wizara imepanga kutoa mikopo kwa Watumishi wa Serikali **150.**

**Ushirikiano na Taasisi za kimataifa Katika Uendelezaji wa Makazi**

63. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kushiriki katika mikutano mbalimbali ya kimataifa yenye lengo la kujenga mahusiano na kubadilishana uzoefu katika usimamizi na uendelezaji makazi nchini. Katika mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kusimamia na kuratibu ushirikiano na taasisi mbalimbali katika uendelezaji wa makazi nchini. Hadi tarehe 15 Mei 2026, Wizara imeshiriki kwenye mikutano sita (**6**) ya Kitaifa na Kimataifa ikiwemo;

i) Mkutano wa kuhitimisha Programu ya Kuimarisha Uwezo wa Ushauri wa Utawala wa Ardhi Barani Afrika (SLGA) uliofadhiliwa na Serikali ya Ujerumani na kuratibiwa na Tume ya Umoja wa Afrika jijini Addis Ababa Agosti, 2025;

ii) Mkutano wa Pili wa Mabadiliko ya Tabianchi Afrika (ACS2), Addis Ababa Septemba, 2025;

iii) Kikao kazi cha uthibitishaji wa Mpango Kazi wa pamoja wa kukabiliana na Maafa yanayohusiana na kuongezeka kwa kina cha maji katika Ziwa Tanganyika katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Burundi, Dar es Salaam, Septemba, 2025;

iv) Kongamano la kimataifa la matumizi ya Akili Mnemba katika kukabiliana na

mabadiliko ya Tabianchi katika nchi zinazoendelea na nchi ya Visiwa Vidogo lililoandaliwa na Umoja wa Mataifa (UNFCCC) uliofanyika Dar es Salaam, Oktoba, 2025;

v) Mkutano wa 30 wa Umoja wa Mataifa wa Mkataba wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (UNFCCC) uliofanyika Belem - Brazil Novemba, 2025;

vi) Jukwaa la Pili la Miji Afrika (The Second African Urban Forum) lililofanyika Nairobi nchini Kenya Aprili, 2026; na

vii) Jukwaa la 13 la Miji Duniani limefanyika Baku-Azarbaijan Mei, 2026.




*Mhe. Dkt. Leonard Akwilapo, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi akiwasilisha hoja ya Serikali ya Tanzania katika Kongamano la Pili la Miji Afrika (The Second African Urban Forum) lililofanyika jijini Nairobi nchini Kenya*

64. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/27, Wizara itaendelea kusimamia na kuratibu ushirikiano na taasisi mbalimbali za Kimataifa kwa lengo la kunufaika na fursa mbalimbali katika nyanja za uendelezaji wa miji na makazi.

**USIMAMIZI NA URATIBU WA SEKTA YA MILKI**

65. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina dhamana ya kusimamia, kuratibu na kuendeleza sekta ya milki nchini ili kuhakikisha soko la milki linaimarika na kuwa na uwazi wa kutosha kwa lengo la kulinda maslahi ya wadau wote wakiwemo mawakala, wamiliki, wawekezaji, waendelezaji na watumiaji wa milki. Kwa mujibu wa Taarifa ya Ukuaji wa Uchumi iliyotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu mwezi Desemba 2025, sekta ya milki imechangia Pato la Taifa kwa asilimia **4.40**. Mafanikio haya yameifanya sekta hii kuwa kivutio muhimu kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi hususan katika miradi ya ujenzi wa majengo ya biashara na nyumba za kupangisha na kuuza.

66. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kuratibu ukamilishaji wa mapendekezo ya kutunga Sheria ya Milki, kuhuisha kanzidata ya mawakala wa milki na waendelezaji milki nchini, kukamilisha kanuni

na miongozo ya uendelezaji milki na kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya milki. Hadi tarehe 15 Mei 2026, mapendekezo ya kutunga Sheria ya Milki yamewasilishwa kwenye Mamlaka husika kwa ajili ya uamuzi. Vilevile, jumla ya Mawakala wa Milki **350** wamejisajili katika kanzidata ya Wizara na waendelezaji milki **100** wametambuliwa. Aidha, Wizara imeendeleza uhusiano wa kikanda na kimataifa kwa kushiriki katika mikutano sita (**6**) ya kikanda na kimataifa iliyolenga kutangaza fursa za uwekezaji zilizopo katika sekta ya milki. Pia, Wizara imeratibu mikutano sita (**6**) ya wadau wa sekta ya milki kwa lengo la kuwatambua na kutoa elimu kuhusu uanzishwaji wa vyama vya mawakala wa milki na kujadili namna bora ya utekelezaji wa shughuli zao.

67. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/27, Wizara itaratibu ukamilishaji wa mapendekezo ya kutunga Sheria ya Milki; kukamilisha kanuni na miongozo ya utambuzi na usajili wa mawakala wa milki, usimamizi wa majengo na nyenzo na uendelezaji milki; kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya milki; kuboresha mahusiano na wadau wa sekta ya milki; na kuhuisha kanzidata ya mawakala wa milki na waendelezaji milki nchini. **Natoa wito kwa wadau wote wa sekta ya milki kushirikiana na Serikali ili kuimarisha sekta ya milki kwa**

**manufaa yao na uchumi wa Taifa letu kwa ujumla.**

## MAPITIO YA SHERIA ZA SEKTA YA ARDHI

68. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kufanya marekebisho ya sheria za sekta ya ardhi baada ya kuidhinishwa kwa Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 (Toleo la mwaka 2023) kwa kuzingatia mabadiliko ya kiuchumi, kijamii na kimazingira. Hadi tarehe 15 Mei 2026, Wizara inaendelea na hatua za marekebisho ya Sheria mbili (**2**) za Sekta ambazo ni Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, Sura ya 116 na Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini, Sura ya 138. Katika mwaka 2026/27, Wizara itafanya marekebisho ya Sheria tatu (**3**) na Kanuni sita (**6**) za sekta ya ardhi kwa kuzingatia maelekezo ya Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 (Toleo la mwaka 2023) na mabadiliko ya kiuchumi, kijamii na kimazingira.

## MIRADI YA MAENDELEO

69. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwa ni pamoja na Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi; Mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu ya Upimaji na Ramani (LDI); na Mradi wa Uimarishaji wa Mipaka ya Kimataifa.

**Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi**

70. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji nchini. Katika mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kupima viwanja **15,000**. Hadi tarehe 15 Mei 2026, jumla ya viwanja **35,311** sawa na asilimia **235.41** vimepangwa na kupimwa katika halmashauri **13** nchini. Katika mwaka 2026/27, Wizara imepanga kupima viwanja **15,000**.

71. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Wizara ilipanga Kuwezesha utekelezaji wa miradi inayohusisha utwaaji wa maeneo na uboreshaji wa miji iliyochakaa katika majiji ya Dar es Salaam, Mwanza, Arusha na Mbeya. Hadi tarehe 15 Mei 2026, Wizara kupitia programu ya KKK imewezesha uandaaji wa Mwongozo wa Programu ya uendelezaji wa maeneo chakavu ya miji (*Guideline for Land Re-Adjustment in Tanzania*). Katika mwaka 2026/27, Wizara itaendelea kuwezesha na kusimamia utekelezaji wa mpango wa kuhuisha maeneo chakavu ya miji.

72. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuziwezesha halmashauri ili kuongeza kasi ya kupanga, kupima na kumilikisha ardhi kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Ardhi (*Plot Development Revolving Fund* - PDRF) ambao moja ya vyanzo

vyake ni marejesho ya fedha shilingi bilioni **50.00** zilizokopeshwa mwaka 2021/22 kwenye halmashauri **57**, Vyuo vya Ardhi vya Tabora na Morogoro, Chuo Kikuu Ardhi na Ofisi ya Ardhi Mkoa wa Iringa (**Jedwali Na. 14**). Hadi tarehe 15 Mei 2026, shilingi bilioni **33.18** zimerejeshwa sawa na asilimia **66.41** ya fedha zilizokopeshwa. Wizara inaendelea kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu- TAMISEMI na Wizara ya Fedha kuchukua hatua madhubuti kwa halmashauri zote ambazo hazijakamilisha kurejesha fedha hizo. **Nitumie fursa hii kuzipongeza halmashauri ambazo zimekamilisha marejesho ya fedha zilizokopeshwa na kuzitaka halmashauri ambazo hazijakamilisha kurejesha mikopo hiyo zifanye hivyo mara moja ili kuziwezesha halmashauri nyingine nchini kunufaika na fursa hiyo.**

**Mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu ya Upimaji na Ramani**

73. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea na utekelezaji wa Mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu ya Upimaji na Ramani (Land Data Infrastructure - LDI) kwa lengo la kurahisisha kazi za upangaji na upimaji nchini. Katika mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kukamilisha ununuzi wa vifaa na kuanza uandaaji wa ramani za msingi za uwiano wa **1:2,500** kwa miji mikuu ya mikoa na uwiano wa **1:25,000** kwa nchi nzima. Hadi

tarehe 15 Mei 2026, Wizara imekamilisha kuandaa viwango na miongozo ya uandaaji wa ramani za msingi zitakazotumika kudhibiti ubora wa ramani zitakazoandaliwa na Mkandarasi na wadau wengine wanaotengeneza ramani. Aidha, Wizara imefanikiwa kumpata mkandarasi atakayeleta ndege maalum itakakayotumika kupiga picha za anga zitakazotumika kutengeneza ramani za msingi za uwiano mkubwa katika maeneo yaliyoainishwa kwenye makao makuu ya mikoa. Katika mwaka 2026/27, Wizara inatarajia kumpata Mkandarasi atakayejenga Vituo vya Kielektroniki vya Upimaji **30** (Continuously Operating Reference Stations - CORS) na kuandaa Ramani za Msingi nchi nzima za uwiano mdogo wa **1:25,000**.

74. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha mradi huu unatekelezwa ipasavyo, Wizara imefanikiwa kupandisha hadhi Kituo cha Taifa cha Ubunifu na Mafunzo ya Teknolojia ya Taarifa za Kijiografia (TNGC) kuwa Chuo cha Mafunzo ya Kati. Chuo hiki kimesajiliwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) kwa ajili ya kutoa mafunzo katika Ngazi ya Astashahada. Chuo hicho kitaongeza uwezo wa wataalamu wa ndani kutekeleza miradi ya sekta ya ardhi na hivyo kuokoa matumizi ya fedha za kigeni zinazotumika kuajiri wataalam kutoka nje ya nchi na kupeleka watalaam nje ya nchi. Katika

mwaka 2026/27, chuo kitaanza kutoa mafunzo kwa wanafunzi **60** katika taaluma za upimaji kwa njia ya satelaiti pamoja na uandaaji ramani kwa kutumia ndege zisizokuwa na rubani (Satelite Survey and Drone Mapping).

**Mradi wa Uimarishaji wa Mipaka ya Kimataifa**

75. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuimarisha mipaka ya kimataifa kwa kujenga na kuongeza alama, kupima, kukarabati alama zilizoharibika, kuandaa ramani za mipaka na kuandaa makubaliano ya uimarishaji wa mipaka. Katika mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kuimarisha sehemu ya mpaka wa kimataifa kati ya Tanzania na Kenya wenye urefu wa kilomita **100** pamoja na mpaka wa Tanzania na Burundi wenye urefu wa kilomita **100**. Hadi tarehe 15 Mei 2026, Wizara imeimarisha Mpaka wa Kimataifa kati ya Tanzania na Kenya kutoka Tarakea Wilaya ya Rombo hadi Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi Wilaya ya Mwanga kwa jumla ya kilomita **106** sawa na asilimia **106** na kufanya jumla ya kilomita zilizoimarishwa kufikia **564** kati ya kilomita **758** za eneo la nchi kavu katika mpaka kati ya Tanzania na Kenya.



*Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii ikipata maelezo kuhusu Uimarishaji Mpaka wa Kimataifa kati ya Tanzania na Kenya katika eneo la Holili Wilaya ya Rombo mkoani Kilimanjaro*



*Muonekano wa mkuza wa Mpaka wa Kimataifa kati ya Tanzania na Kenya uliopo eneo la Holili Wilaya ya Rombo mkoani Kilimanjaro*

76. ***Mheshimiwa Spika,*** uimarishaji wa mipaka hutegemea makubaliano baina ya nchi na nchi. Ili kuwezesha hayo, Wizara imeshiriki katika mikutano ambayo ni Tume ya Pamoja ya Kudumu ya Ulinzi na Usalama- JPCDS kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Msumbiji; na Kamati ya Pamoja ya Wataalamu wa uimarishaji mpaka katika ziwa Tanganyika kati ya Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo- DRC, Tanzania na Zambia yenye lengo la kujadili namna ya kutekeleza zoezi la uimarishaji wa mipaka. Aidha, mafunzo ya pamoja ya wataalamu ya uimarishaji mpaka wa kimaitaifa kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Burundi yanayohusu uhakiki na uimarishaji wa mpaka katika eneo la Mto Malagarasi yamefanyika.

77. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mujibu wa Mkataba wa Kimataifa wa Sheria ya Bahari, nchi zote zinazopakana na bahari na zilizoridhia mkataba huo kabla ya mwaka 1999, zilipewa fursa ya kuwasilisha maombi ya eneo la nyongeza mbele ya Umoja wa Mataifa. Mwaka 2012 Tanzania iliwasilisha maombi ya kuongezewa eneo Nje ya Ukanda wa Kiuchumi Baharini kwenye Tume ya Umoja wa Mataifa inayoshughulikia mipaka ya Baharini (Commission of the Limits of the Continental Shelf). Eneo linaloombwa linakadiriwa kuwa na ukubwa wa kilomita za

mraba **61,000** (sawa na ukubwa wa mikoa ya Tanga, Pwani na Dar es Salaam kwa pamoja). Umuhimu wa eneo linaloombwa ni kuiwezesha nchi kunufaika na rasilimali zinazoweza kupatikana katika eneo husika.

78. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Tanzania ilipata fursa ya kutetea andiko hilo mbele ya Tume ya Umoja wa Mataifa inayoshughulikia Mipaka Baharini (Commission on the Limits of Continental Shelf – CLCS) Jijini New York, Marekani. Kufuatia utetezi huo, Tume ilitoa maoni na mapendekezo ambayo yanaendelea kufanyiwa kazi na Kikosi Kazi kwa kuzingatia taarifa za kijiolojia, jiofizikia, jiodesia, kihaidrografia na sheria za mipaka ya Bahari. Andiko lililoboreshwa litawasilishwa mbele ya Tume mwezi Julai mwaka huu.

79. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/27, Wizara imepanga kuendelea kuimarisha sehemu ya mpaka wa Tanzania na Kenya yenye urefu wa kilomita **140**; kuimarisha sehemu ya mpaka wa Tanzania na Burundi yenye urefu wa kilomita **70**; kupima na kuimarisha kilomita **100** za Mipaka ya Kimataifa kwenye maji; kukamilisha maboresho ya andiko la utetezi kuhusu Eneo la Nyongeza Nje ya Ukanda wa Kiuchumi Baharini; na kuwezesha ukusanyaji na uchakataji wa data zinazohusiana na maji.

## TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA

80. ***Mheshimiwa Spika,*** miongoni mwa majukumu ya Wizara ni kuratibu na kusimamia shughuli za taasisi zilizo chini yake. Taasisi hizo ni Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi; Shirika la Nyumba la Taifa; Bodi ya Usajili wa Wataalam wa Mipangomiji, Bodi ya Usajili wa Wathamini, Baraza la Taifa la Wapima Ardhi na Vyuo vya Ardhi vya Tabora na Morogoro.

### Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi

81. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Tume imeendelea kuandaa, kuratibu na kusimamia utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi katika maeneo mbalimbali nchini; kufanya tafiti zinazohusu matumizi ya ardhi; pamoja na kufuatilia, kutathmini na kuhakikisha uzingatiaji wa mipango hiyo. Utekelezaji wa majukumu haya unazingatia Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, Sura ya 116; na Mpango Mkakati wa Tume (2021/22–2025/26) uliozingatia Mpango wa Matumizi ya Ardhi wa Taifa (2013–2033).

82. ***Mheshimiwa Spika,*** upangaji wa matumizi ya ardhi ni nyenzo muhimu katika kuhakikisha matumizi endelevu ya rasilimali ardhi hasa katika muktadha wa ongezeko la watu, mifugo

na mahitaji mbalimbali ya ardhi ikiwemo kilimo, malisho na makazi. Aidha, huchangia kulinda usalama wa milki za ardhi na kudhibiti migogoro ya ardhi nchini. Kupitia mipango hii, maeneo hutengwa kwa matumizi mbalimbali kama vile kilimo, ufugaji, uwekezaji na makazi ili kuzuia muingiliano wa matumizi hususan katika maeneo nyeti kama shoroba za wanyamapori, mazalia ya wanyamapori, vyanzo vya maji, misitu ya hifadhi, mapori tengefu, mapori ya akiba pamoja na ardhi ya uwekezaji na malisho. Mipango hii huandaliwa na kutekelezwa katika ngazi mbalimbali kuanzia Taifa, kanda, mikoa, wilaya na vijiji.



*Mwenyekiti wa Kijiji cha Namagondo kilichopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe mkoani Mwanza, akiwasilisha Mpango wa Matumizi ya Ardhi na Mpangokina wa kijiji mbele ya Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhe. Kaspar Kaspar Mmuya.*

**Uandaaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi**

83. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Tume ilipanga kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji **240** kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi tarehe 15 Mei 2026, mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji **253** katika halmashauri za wilaya **24** nchini imeandaliwa sawa na asilimia **105.42** ya lengo na kufanya jumla ya vijiji vilivyopangwa kufikia **4,925** kati ya vijiji **12,333** vilivyopo nchini (**Jedwali Na. 15**). Kati ya vijiji vilivyoandaliwa mipango ya matumizi ya ardhi, vijiji **2,750** sawa na asilimia **55.83** vimepangwa katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi mahiri wa **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**. Katika mwaka 2026/27, Tume kwa kushirikiana na wadau itaandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji **1,492**. **Napenda kutumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuongeza tengeo la bajeti kwa ajili ya kuongeza kasi ya uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi nchini. Aidha, tengeo hilo litawezesha upangaji wa matumizi ya ardhi ya vijiji vingi kwa muda mfupi ikilinganishwa na kipindi kilichopita. Hii inadhihirisha azma ya Mheshimiwa Rais ya kumaliza migogoro ya matumizi ya ardhi nchini na kurejesha tabasamu kwa Watanzania**

84. ***Mheshimiwa Spika***, uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi uliotekelezwa na Tume umewezesha uhakiki na utatuzi wa migogoro ya mipaka ya vijiji **223** katika halmashauri za wilaya **20** ambazo ni Nanyumbu (**13**), Mtwara (**19**), Mtama (**5**), Bahi (**10**), Nyang'hwale (**6**), Mbogwe (**4**), Sikonge (**17**), Nzega (**44**), Simanjiro (**2**), Kilolo (**3**), Gairo (**19**), Masasi (**13**), Mbeya (**2**), Misungwi (**10**), Kisarawe (**6**), Muheza (**11**), Busega (**10**), Morogoro (**12**), Mpwapwa (**10**) na Kiteto (**7**). Aidha, uchambuzi umebaini kuwa miongoni mwa vyanzo vya migogoro hiyo ni mgongano wa maslahi na mgawanyo wa rasilimali kutokana na kuanzishwa kwa maeneo mapya ya kiutawala; kutokuwepo kwa alama za kudumu za mipaka; na uelewa mdogo wa wananchi kuhusu mipaka ya vijiji. Hali hii husababisha migongano ya matumizi ya ardhi na uvamizi wa maeneo yaliyohifadhiwa ikiwemo; hifadhi za wanyamapori, vyanzo vya maji, misitu ya hifadhi, mapori ya akiba na mapori tengefu.

85. ***Mheshimiwa Spika,*** uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi nchini unaratibiwa na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji. Hivyo, ni wajibu wa Mamlaka za Upangaji kuhakikisha zinaweka masuala ya mipango ya matumizi ya ardhi kwenye vipaumbele vyao. **Natoa wito kwa Mamlaka za Upangaji**

**kuhakikisha zinatenga fedha kwa ajili ya mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji pamoja na kutoa elimu kwa wananchi kuhakikisha wanazingatia mipango ya matumizi ya ardhi iliyoandaliwa kwenye maeneo yao.**

**Uandaaji wa Mipangokina**

86. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume imeendelea kutekeleza jukumu lake la kuwezesha uandaaji wa Mipangokina katika vitovu vya vijiji na maeneo ya mashamba kwa lengo la kurahisisha utoaji wa Hati za Hakimiliki ya Kimila. Katika mwaka 2025/26, Tume ilipanga kuandaa Mipangokina sita (**6**) pamoja na kutoa Hati za Hakimiliki ya Kimila **2,000** kwa maeneo ya makazi na mashamba. Hadi tarehe 15 Mei 2026, jumla ya Mipangokina **34** imeandaliwa katika maeneo ya makazi na mashamba kwenye halmashauri za wilaya nane (**8**) nchini. Utekelezaji huu umewezesha kutolewa kwa Hati za Hakimiliki ya Kimila **6,231** sawa na asilimia **316.05** ya lengo katika wilaya mbalimbali zikiwemo Rungwe (**739**), Ushetu (**1,022**), Sikonge (**1,156**), Urambo (**333**), Kaliua (**323**), Nyang'hwale (**838**), Ukerewe (**1,308**) na Mlimba (**512**). Katika mwaka 2026/27, Tume itaandaa Mipangokina katika vijiji **145** kwenye maeneo ya makazi na mashamba itakayowezesha utoaji wa Hati za Hakimiliki ya Kimila **87,000**.

**Kuzijengea Uwezo Mamlaka za Upangaji**

87. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Tume ilipanga kuzijengea uwezo Mamlaka za Upangaji **248** katika ngazi za wilaya na vijiji pamoja na kutoa elimu kuhusu sheria za ardhi, miongozo na taratibu za uandaaji, utekelezaji na usimamizi wa mipango ya matumizi ya ardhi nchini. Hadi tarehe 15 Mei 2026, Tume imefanikiwa kuzijengea uwezo Mamlaka za Upangaji **277** sawa na asilimia **111.69** ya lengo zikiwemo halmashauri za vijiji **253** na halmashauri za wilaya **24** kuhusu masuala ya uandaaji, usimamizi na utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi yenye wajumbe **21,721** wa Kamati za Usimamizi wa Ardhi ngazi ya wilaya (**192**), wajumbe wa halmashauri za vijiji (**5,819**), Wajumbe wa Kamati za Usimamizi wa Ardhi ya Vijiji (**2,024**), Wajumbe wa Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji (**11,771**), Wajumbe wa Kamati za Uhakiki wa Mipaka (**1,771**) pamoja na Wajumbe wa Kamati za Uhakiki wa Maslahi ya Ardhi (**144**). Aidha, elimu ilitolewa kuhusu usuluhishi wa migogoro ya ardhi, uhifadhi wa mazingira, ulinzi wa mapitio ya wanyamapori, vyanzo vya maji, uzingatiaji wa matumizi yaliyopangwa ya ardhi pamoja na uhifadhi wa misitu ili kuimarisha ustahimilivu dhidi ya mabadiliko ya tabianchi. **Natoa wito kwa wadau wa kisekta na Mamlaka za Upangaji kuhakikisha maeneo yaliyopangwa**

**yanaandaliwa Mipangokina na kuwekewa miundombinu ili kuepusha uvamizi na migogoro ya ardhi. Aidha, mamlaka za upangaji ziendelee kuchukua hatua za kisheria kwa wale wote wanaokiuka mipango ya matumizi ya ardhi iliyopo.**

88. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuendana na kasi ya mabadiliko na maendeleo ya teknolojia katika uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi na kuwezesha upatikanaji wa taarifa za matumizi ya ardhi kwa wakati, matumizi ya teknolojia za kisasa hayakwepeki. Kutokana umuhimu huo, Wizara kupitia Tume inaendelea kuhuisha kanzidata ya mipango ya matumizi ya ardhi na Mfumo wa Uandaaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi. Mfumo huu utawawezesha wadau kusajili mipango ya matumizi ya ardhi ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa za mipango ya matumizi ya ardhi na hivyo kuwezesha uratibu na usimamizi Madhubuti wa wadau wote wanaohusika na upangaji wa matumizi ya ardhi nchini. Hadi tarehe 15 Mei 2026, jumla ya Mipango ya Matumizi ya ardhi ya vijiji **590** imehifadhiwa kwenye Mfumo na kufanya kuwa na jumla ya mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji **2,584** iliyohifadhiwa kwenye mfumo. Aidha, mafunzo ya uandaaji wa Mipangokina ya matumizi ya ardhi kidijiti yametolewa kwa wajumbe **64** wa Timu za Usimamizi wa Ardhi za

Wilaya (PLUM Team) za halmashauri za wilaya nane (**8**) ambazo ni Urambo, Kaliua, Sikonge, Ushetu, Nyangh'wale, Rungwe, Ukerewe na Mlimba.

**Ufuatiliaji na Tathmini ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi**

89. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Tume ilipanga kufanya ufuatiliaji na tathmini ya mipango ya matumizi ya ardhi katika vijiji **40**, hususan katika maeneo ya miradi ya kimkakati (SGR, EACOP, JNHPP), wilaya za mipakani na vijiji vyenye migogoro. Hadi tarehe 15 Mei 2026, zoezi limefanyika katika vijiji **33** ndani ya Halmashauri **11** za Handeni (**4**), Wanging'ombe (**4**), Tarime (**4**), Meatu (**4**), Shinyanga (**5**), Sumbawanga (**1**), Musoma (**1**), Butiama (**1**), Makete (**1**), Chato (**4**) na Mbarali (**4**). Matokeo yanaonesha kuwa utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi umechangia kupungua kwa migogoro ya ardhi kwa wastani wa asilimia **71**, kuimarika kwa uhifadhi wa mazingira kwa asilimia **79** na kufikiwa kwa asilimia **83** ya utekelezaji wa matumizi yaliyopangwa kwa maeneo ya makazi, kilimo, huduma za jamii na miundombinu. Mafanikio haya yanatokana na uwepo wa mipango elekezi pamoja na ufuatiliaji katika maeneo ya miradi ya kimkakati.

90. ***Mheshimiwa Spika,*** tathmini pia imebaini kuwa utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi katika maeneo ya malisho na misitu ya hifadhi bado uko chini ya kiwango kinachotarajiwa kutokana na changamoto za usimamizi, uvamizi wa ardhi na ukosefu wa mifumo endelevu ya kiuchumi. Katika mwaka 2026/27, Tume itafanya ufuatiliaji na tathmini ya mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji **232** katika miradi ya kimkakati (SGR, EACOP, JNHPP), vijiji vilivyopo katika wilaya za mipakani mwa Tanzania na nchi jirani pamoja na vijiji vyenye migogoro ya matumizi ya ardhi ili kuongeza uzalishaji. Vilevile, Tume itaimarisha ufuatiliaji wa kidijiti kwa kutumia mifumo ya taarifa za kijiografia (GIS), kuanzisha viashiria mahsusi vya kupima utendaji wa mipango ya matumizi ya ardhi na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu matumizi endelevu ya maeneo ya malisho na misitu ili kuongeza tija, mapato na kupunguza migogoro.

**Shirika la Nyumba la Taifa**

91. ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika la Nyumba la Taifa lina jukumu la kujenga nyumba za makazi na majengo mengine kwa ajili ya kuuza na kupangisha; kujenga majengo kulingana na mipango iliyoidhinishwa na Serikali; kuzalisha na kuwezesha uzalishaji wa vifaa vya ujenzi; kusimamia milki za majengo; kufanya ukarabati wa nyumba; kukusanya kodi ya pango la nyumba za Shirika; kutoa

huduma ya ushauri elekezi; upangaji wa maeneo ya ujenzi wa nyumba; na kutekeleza kazi za ukandarasi wa majengo. Majukumu hayo yanatekelezwa kwa kuzingatia Mpango Mkakati wa Shirika wa miaka 11 (2015/16 – 2025/26).

92. ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika la Nyumba la Taifa limeendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa nyumba **5,000** wa Samia Housing Scheme unaotarajiwa kugharimu jumla ya shilingi bilioni **466**. Katika mwaka 2025/26, Shirika lilipanga kuendelea na awamu ya pili ya utekelezaji wa Mradi wa Samia Housing Scheme kwa kujenga nyumba **908** katika maeneo mbalimbali nchini. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi tarehe 15 Mei 2026, ujenzi wa nyumba **68** za makazi eneo la Iyumbu (Dodoma) umekamilika hivyo kufanya jumla ya nyumba zilizokamilika kufikia **628.** Aidha, ujenzi wa nyumba **260** katika eneo la Mtoni Kijichi umefikia asilimia **30**, ujenzi wa nyumba **160** eneo la Medeli (Dodoma) umefikia asilimia **25** na nyumba **100** Iyumbu awamu ya pili imefikia asilimia **5.** Kadhalika, maandalizi ya ujenzi wa nyumba katika maeneo ya Njedengwa (Dodoma), Kawe na 105 Boulevard Residence (Dar es Salaam) yanaendelea.



*Mradi wa nyumba za Shirika la Nyumba la Taifa wa Samia Housing Scheme uliopo eneo la Kawe jijini Dar es Salaam*



*Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) katika eneo la Kijichi jijini Dar es Salaam*

93. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Wizara kupitia Shirika la Nyumba la Taifa ilipanga kukamilisha ujenzi wa miradi iliyokuwa imesimama katika Mkoa wa Dar es Salaam ikiwemo nyumba **422** katika Mradi wa Kawe 711 wenye thamani ya shilingi bilioni **169**. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, ujenzi wa mradi huu umefikia asilimia **85** ya utekelezaji na unatarajiwa kukamilika ifikapo tarehe 30 Juni 2026. Aidha, ujenzi wa nyumba **196** katika Mradi wa *Golden Premier Residence (GPR)* wenye thamani ya shilingi bilioni **127** umefikia asilimia **50** na unatarajiwa kukamilika mwaka 2027. Vilevile, ujenzi wa mradi wa Kiwanja Na. 300 *Regent Estate* upo katika hatua ya zabuni.

94. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Wizara kupitia Shirika la Nyumba la Taifa ilipanga kuendelea na usimamizi wa ujenzi wa miradi **21** ya ubia yenye thamani ya shilingi bilioni **351** na kukaribisha wawekezaji wengine kutoka sekta binafsi ili kufanya uendelezaji wa majengo ya biashara na makazi kupitia Sera ya Ubia. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa usimamizi wa miradi hii unaendelea ambapo miradi mitatu imekamilika na miradi mingine iliyobaki imefikia wastani wa asilimia **56** ya utekelezaji na inatarajiwa kukamilika mwaka 2027. Aidha, maombi mapya ya miradi

**68** yenye thamani ya shilingi bilioni **607** yapo katika hatua mbalimbali ambapo miradi **38** inatarajiwa kuanza mwezi Juni 2026 na miradi **30** ipo katika hatua mbalimbali za uchambuzi.

95. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Wizara kupitia Shirika la Nyumba la Taifa ilipanga kuendelea na utwaaji wa miradi ya ubia iliyosimama kwa muda mrefu ili iweze kutekelezwa na Shirika lenyewe kwa mujibu wa mikataba. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kati ya miradi ya ubia **24** iliyokuwa imesimama, miradi **13** imekamilika na miradi minne (**4**) inaendelea kusimamiwa na Shirika ili wabia waikamilishe, miradi mitatu (**3**) imetwaliwa na utekelezaji wake utaendelea kuanzia Julai, 2026. Vilevile, miradi mingine minne (**4**) inatarajiwa kutwaliwa ifikapo Juni 2026 katika mikoa ya Mwanza (**2**), Dar es Salaam (**1**) na Iringa (**1**).

96. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Wizara kupitia Shirika lilipanga kuendelea na ujenzi wa miradi ya majengo ya biashara katika mikoa mbalimbali nchini ikiwamo Meru View shops (Arusha), Tabora Commercial Complex (Tabora), Singida 2F Plaza (Singida), Mkwakwani Commercial Complex (Tanga), Kashozi Commercial Complex (Kagera), Uluguru Plaza (Morogoro), Iringa Commecial Complex (Iringa) na Uhuru shopping centre- Ilala (Dar es Salaam). Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, ujenzi wa

mradi wa Meru View Shops (Arusha) umefikia asilimia **52**; Tabora Commercial Complex (Tabora) umefikia asilimia **46**; Singida 2F Plaza (Singida) umefikia asilimia **85**; Mkwakwani Commercial Complex (Tanga) umefikia asilimia **40**; Kashozi Commercial Complex (Kagera) umefikia asilimia **65**; Uluguru Plaza (Morogoro) umefikia asilimia **42**; na Iringa Commercial Complex (Iringa) umefikia asilimia **40**.



*Mradi wa ujenzi wa jengo la biashara katika eneo la Mkwakwani mkoani Tanga (Mkwakwani Commercial Complex)*

97. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Wizara kupitia Shirika la Nyumba la Taifa ilipanga kuanza ujenzi wa miradi mipya

katika miji na halmashauri mbalimbali ikiwemo jengo la matumizi mchanganyiko mkoani Ruvuma, majengo ya biashara na ofisi – Masasi, Lindi, Usa River na Ngarenaro. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa ujenzi wa jengo la matumizi mchanganyiko mkoani Ruvuma uko katika hatua ya ujenzi wa msingi, miradi ya Usa River na Ngarenaro maandalizi ya ujenzi yako hatua za mwisho. Aidha, Shirika limekamilisha ujenzi wa majengo ya biashara na ofisi ya Mtanda (Lindi), Zongomela (Kahama) na Masasi Commercial Complex (Masasi- Mtwara). Vilevile, ujenzi wa maghala tisa (**9**) kwa ajili ya kupangisha katika Manispaa ya Mtwara umeanza ambapo awamu ya kwanza ya ujenzi wa maghala matatu (**3**) unaendelea na umefikia asilimia **78**.

98. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Wizara kupitia Shirika la Nyumba la Taifa ilipanga kuendelea na kuanza upembuzi yakinifu wa ujenzi wa miradi ya vitovu vya miji vikiwemo Mwashiwawala (Songwe), Kwala (Pwani), Urafiki na Salama Creek (Dar es Salaam) ifikapo Juni, 2026. Nalitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, upembuzi yakinifu katika miradi ya Mwashiwawala na Usa River, Salama Creek umekamilika. Aidha, upembuzi yakinifu katika eneo la Kwala na Urafiki unaendelea na utakamilika mwezi Juni, 2026.

99. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26 Wizara kupitia Shirika la Nyumba la Taifa ilipanga kuendelea kukusanya madeni ya kodi ya nyumba, miradi ya ukandarasi, uuzaji wa nyumba, viwanja na madeni mengineyo. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi tarehe 15 Mei 2026, Shirika limepunguza madeni hayo kutoka shilingi bilioni **27.98** mwaka 2024/25 hadi shilingi bilioni **19** mwaka 2025/26. **Nitumie fursa hii kuwataka wadaiwa wote kutekeleza wajibu wao wa kulipa madeni yao kabla Shirika halijachukua hatua kali za kisheria.**

100. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Wizara kupitia Shirika la Nyumba la Taifa ilipanga kukarabati nyumba za Shirika **1,600**. Hadi tarehe 15 Mei 2026, Shirika limekarabati nyumba **1,283** sawa na asilimia **80** ya lengo. Aidha, ukarabati wa nyumba **317** uko katika hatua za mwisho za utekelezaji.

101. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Wizara kupitia Shirika la Nyumba la Taifa ilipanga kuendelea na ujenzi wa miradi ya ukandarasi na ushauri elekezi. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa ujenzi wa majengo nane (**8)** ya Ofisi za Serikali katika Mji wa Serikali Mtumba umekamilika na kukabidhiwa kwa washitiri. Aidha, usanifu na ujenzi wa jengo la soko la madini (Tanzanite) eneo la Mirerani Manyara umekamilika**.** Vilevile, ujenzi

wa miradi ya ukandarasi na utaalamu elekezi wa majengo ya Ofisi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania (TCRA) jijini Dodoma umefika asilimia **73** na Zanzibar umefikia asilimia **50**. Kadhalika, Shirika limeanza kutoa ushauri elekezi katika miradi mipya ya ujenzi wa Makao Makuu ya Wakala wa Barabara Vijijini (TARURA) na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) jijini Dodoma.

102.***Mheshimiwa Spika,*** ili kuwezesha upatikanaji wa nyumba za gharama nafuu, Shirika linaendelea kukamilisha maandalizi ya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu kwa awamu ambapo utekelezaji utaanza mwaka 2026/27 katika mradi wa Salama Creek (Kigamboni, Dar es Salaam), Sabasaba (Morogoro), Iyumbu (Dodoma) na Buswelu (Mwanza). **Natoa wito kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa na mamlaka zinazohusika na uwekaji wa miundombinu ya umeme, maji na barabara kuunga mkono jitihada za Shirika kwa kuwezesha upatikanaji wa ardhi na miundombinu ili kupunguza gharama za ujenzi wa nyumba katika maeneo ya utekelezaji.**

103.***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/27, Shirika limepanga kutekeleza kazi zifuatazo: -

i) Kuendelea na ujenzi wa nyumba katika Mradi wa nyumba **5,000** wa *Samia Housing Scheme* katika maeneo ya Mtoni

Kijichi na Kawe (Dar es Salaam) na Medeli na Iyumbu (Dodoma). Aidha, Shirika litaanza ujenzi wa nyumba katika maeneo ya Njedengwa (Dodoma), Urafiki (Dar es Salaam), Sokoine complex (Mtaa wa Azimio- Arusha) na Makongoro (Mwanza);

ii) Kuanza ujenzi wa nyumba **800** za gharama nafuu kwa awamu katika mradi wa Salama Creek (Kigamboni, Dar es Salaam), Sabasaba (Morogoro), Iyumbu (Dodoma) na Buswelu (Mwanza);

iii) Kuendelea na ujenzi wa nyumba **196** katika mradi wa Golden Premier Residence (GPR) na Kiwanja Na.300 Regent Estate;

iv) Kuendelea na usimamizi wa ujenzi wa miradi ya ubia na kukaribisha wawekezaji wengine kutoka sekta binafsi na zile za Umma ili kufanya uendelezaji wa majengo ya biashara na makazi kupitia Sera ya Ubia;

v) Kuendelea kukamilisha ujenzi wa miradi ya majengo ya biashara katika mikoa mbalimbali nchini ikiwemo Meru view shops, Ngarenaro na Usa River (Arusha), Tabora Commercial Complex (Tabora), Mkwakwani Commercial Complex (Tanga), Uluguru Plaza (Morogoro), Iringa Commercial Complex (Iringa), Songea Commercial Complex (Ruvuma); Bukoba Complex (Kagera), 17A mwenge na 1K

Market Street (Singida), Uganda Avenues na RAS Kilomoni (Dar es Salaam).

vi) Kuendelea na upembuzi yakinifu wa ujenzi wa miradi ya vitovu vya miji ikiwemo Kwala (Pwani) na Salama Creek (Dar es Salaam);

vii) Kuendelea kutekeleza mpango wa ukarabati wa nyumba za Shirika **2,200**; na

viii) Kutekeleza miradi ya ukandarasi na Ushauri elekezi inayoendelea na mingine itakayojitokeza.

## BODI ZA USAJILI WA WATAALAM WA FANI ZA ARDHI

104. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara pia inasimamia utekelezaji wa shughuli za Bodi mbalimbali za wataalam wa sekta ya ardhi. Bodi hizo ni Bodi ya Usajili wa Wataalam wa Mipangomiji, Bodi ya Usajili wa Wathamini na Bodi ya Usimamizi na Usajili wa Wapima Ardhi. Majukumu ya Bodi hizi ni kusajili wataalam wa sekta na kampuni za kitaalam, kusimamia weledi wa wataalam na kusimamia maadili ya kitaaluma.

## Bodi ya Usajili wa Wataalam wa Mipangomiji

105.***Mheshimiwa Spika***, Bodi ya Usajili wa Wataalam wa Mipangomiji ilianzishwa kwa Sheria ya Usajili wa Wataalam wa Mipangomiji, Sura ya 426. Lengo kuu ni kusajili, kusimamia maadili na taaluma pamoja na kuishauri Serikali kuhusu masuala yanayohusu taaluma ya mipangomiji nchini. Katika mwaka 2025/26, Bodi ilipanga kusajili Wataalam na Kampuni za Mipangomiji zitakazokidhi vigezo ili kuimarisha utendaji kazi pamoja na kusimamia na kufuatilia utendaji kazi katika mikoa **26**. Hadi tarehe 15 Mei 2026, Bodi imesajili wataalam **98** na kampuni tatu (**3**) na hivyo kufikia jumla ya watalaam **610** na kampuni **102** zilizosajiliwa tangu Bodi ilipoanzishwa. Aidha, ufuatiliaji wa utendaji kazi umefanyika katika mikoa **15** ya Dar es salaam, Mwanza, Iringa, Njombe, Arusha, Kilimanjaro, Singida, Tabora, Kigoma, Mara, Simiyu, Ruvuma, Songwe, Mbeya na Mtwara na kazi inaendelea katika mikoa **11**. Katika mwaka 2026/27, Bodi imepanga kusajili Wataalam wa Mipangomiji **96** na Kampuni tisa (**9**) na kuendelea kusimamia na kufuatilia utendaji kazi na uzingatiaji wa Sheria ya Usajili wa Wataalam wa Mipangomiji katika mikoa **26**.

**Bodi ya Usajili wa Wathamini**

106.***Mheshimiwa spika,*** Bodi ya Usajili wa Wathamini ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini, Sura ya 138 kwa ajili ya kusajili Wathamini na kudhibiti kazi za uthamini nchini. Aidha, Bodi inahusika na utoaji wa leseni kwa wataalam wa uthamini, kusimamia nidhamu na maadili ya taaluma na kuhimiza maendeleo ya elimu na uzoefu katika tasnia ya uthamini.

107.***Mheshimiwa spika,*** katika mwaka 2025/26, Bodi ya Usajili wa Wathamini ilipanga kusajili wathamini **150** katika ngazi zote, kutengeneza mfumo wa TEHAMA kwa ajili ya kurahisisha shughuli za Bodi, kufanya mapitio ya mitaala na kukusanya shilingi bilioni **1.70** kutoka kwenye vyanzo vyake vya mapato. Hadi tarehe 15 Mei 2026, Bodi imekamilisha usanikishaji wa mfumo, mapitio ya mitaala na kusajili Wathamini **145** sawa na asilimia **96.67** ya lengo. Kati ya hao, Wathamini wawili (**2**) katika usajili kamili, Wathamini **99** katika ngazi ya usajili wa awali, Wathamini **44** wameorodheshwa kama Wathamini Wasaidizi na Kampuni tatu (**3**) za uthamini zimesajiliwa. Aidha, Bodi ilipokea na kuamua masuala **10** ya kimaadili na nidhamu. Kati ya hayo, masuala matano (**5**) yanahusu Wathamini na matano (**5**) yanahusu kampuni za uthamini. Vilevile, Bodi ilikusanya shilingi

bilioni **1** kutoka kwenye ada za usajili, ada ya kila taarifa ya uthamini na ada ya mitihani ya kitaaluma sawa na asilimia **58.82** ya lengo. Katika mwaka 2026/27, Bodi imepanga kusajili Wathamini **150** katika ngazi mbalimbali za usajili na Kampuni **10** za Uthamini. Pia, Bodi itaendelea kusimamia maadili ya kazi kwa Wathamini na Kampuni zilizosajiliwa ili kuhakikisha kazi za uthamini zinafanyika kwa weledi na ufanisi. Aidha, Bodi imepanga kukusanya shilingi bilioni **1.40**.

**Bodi ya Usimamizi na Usajili wa Wapima Ardhi**

108. ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi ya Usimamizi na Usajili wa Wapima Ardhi inakuza na kusimamia tasnia ya upimaji ardhi nchini. Katika mwaka 2025/26, Bodi ilipanga kusajili Wapima Ardhi **100** na kutoa leseni kwa kampuni za upimaji **30**. Hadi tarehe 15 Mei 2026, Wapima Ardhi **93** wamesajiliwa sawa na asilimia **93** ya lengo na hivyo kuwa na jumla ya Wapima Ardhi **920** waliosajiliwa nchini. Aidha, kampuni **10** zimesajiliwa sawa na asilimia **33.33** ya lengo na hivyo kufanya Kampuni za Upimaji Ardhi zilizosajiliwa kufikia **138**. Vilevile, Bodi imeendelea kuandaa na kutoa mafunzo ya kitaalam kwa Wapima Ardhi kupitia semina, mikutano na makongamano mbalimbali ya kitaaluma ambapo Wapima Ardhi **250** walishiriki mafunzo hayo. Kadhalika, Bodi imeendelea kuchukua hatua kwa Wapima Ardhi

na Kampuni za Upimaji Ardhi zilizobainika kukiuka maadili ya taaluma ya upimaji ardhi ambapo kampuni mbili (**2**) zimepewa onyo. Katika mwaka 2026/27, Bodi imepanga kusajili Wapima Ardhi **100** na kutoa leseni kwa Kampuni za Upimaji Ardhi **20**.

## VYUO VYA ARDHI TABORA NA MOROGORO

109.***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inasimamia Vyuo vya Ardhi Tabora na Morogoro ambavyo hutoa mafunzo ya muda mrefu katika fani mbalimbali za ardhi, kufanya utafiti katika fani za sekta ya ardhi na kutoa ushauri wa kitaalam katika masuala ya ardhi.

110.***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Chuo cha Ardhi Tabora kilipanga kudahili wanafunzi **1,580**; kujenga sehemu ya uzio yenye urefu wa mita **410** kati ya mita **1,331**; na kukamilisha ujenzi wa kumbi mbili (**2**) za mihadhara (Lecture theatres) zenye uwezo wa kubeba wanafunzi **700** kwa wakati mmoja. Hadi tarehe 15 Mei 2026, wanafunzi **1,138** sawa na asilimia **85.49** wamedahiliwa. Aidha, ujenzi wa uzio wenye urefu wa mita **410** umekamilika na ujenzi wa kumbi mbili (**2**) za mihadhara (Lecture theatres) umefikia asilimia **65**. Katika mwaka 2026/27, Chuo kimepanga kudahili wanafunzi **1,500** katika fani tano (**5**) zinazotolewa na Chuo; kuendelea kuboresha

miundombinu ya kujifunzia na kufundishia; kuhuisha mitaala ya kozi za *Geographical Information System* na *Environmental Management* na kuanzisha mitaala mipya ya *Geomatics* pamoja na *Regional and Rural Planning*; kununua mashine ya kuchapisha makala kwa ajili ya kiwanda cha uchapishaji; na kuendelea na ujenzi wa sehemu ya uzio wa Chuo yenye urefu wa mita **410** kati ya mita **921** zilizobaki.



*Mhe. Dkt. Leonard Akwilapo, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi akielezwa hatua za upimaji kwa vitendo wakati wa Mahafali ya Chuo cha Ardhi Tabora (ARITA)*



*Mhe. Dkt. Leonard Akwilapo, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi akipokea zawadi ya picha ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliyochorwa na Mwanafunzi wa Chuo cha Ardhi Tabora (ARITA) wakati wa mahafali ya chuo hicho*

111.***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Chuo cha Ardhi Morogoro, kilipanga kudahili wanafunzi **768**; kujenga vyumba viwili (**2**) vya madarasa; kuimarisha Maabara ya Kompyuta; kujenga uzio katika eneo la chuo; na kufanya ukarabati wa majengo. Hadi tarehe 15 Mei 2026, wanafunzi **574** wamedahiliwa sawa na asilimia **74.74** ya lengo. Aidha, ujenzi wa vyumba viwili (**2**) vya madarasa umefikia

asilimia **60**. Vilevile, Chuo kinaendelea na ujenzi wa sehemu ya uzio yenye urefu wa mita **120** kati ya mita **587** na uimarishaji wa Maabara ya Kompyuta unaendelea. Kadhalika, Chuo kimeboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia kwa kukarabati mabweni mawili (**2**) ya wanafunzi na jengo la Zahanati ya Chuo. Katika mwaka 2026/27, Chuo kimepanga kudahili jumla ya wanafunzi **800**; kuboresha miundombinu pamoja na kuongeza matumizi ya TEHAMA; kutekeleza miradi ya ushauri wa kitaalamu; kupanda miti **1,000**; na kujenga uzio wenye urefu wa mita **120** kati ya **467** zilizobaki.

## UTAWALA NA RASILIMALIWATU

112. ***Mheshimiwa Spika,*** Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu ni nguzo muhimu katika usimamizi na utekelezaji wa majukumu ya Wizara hasa katika maeneo yanayohusiana na masuala ya uendeshaji wa Ofisi, ajira, maendeleo ya kitaaluma, usimamizi wa utendaji kazi na masuala ya ustawi wa watumishi. Katika mwaka 2025/26, Wizara imepokea watumishi **483** wa ajira mpya ambao wameongeza tija na ufanisi, imejaza nafasi nane (**8**) za uongozi na inatarajia kuwapandisha vyeo watumishi **468** na kubadilisha kada watumishi nane (**8**). **Naomba nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri**

**ya Muungano wa Tanzania kwa kutupatia watumishi wapya ambao wataongeza tija na ufanisi katika utoaji wa huduma za sekta ya ardhi nchini.**

113. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilipanga kuwawezesha watumishi kushiriki mafunzo ya muda mfupi na mrefu ambapo hadi tarehe 15 Mei 2026, watumishi **1,288** wamepatiwa mafunzo. Kati ya hao, watumishi **65** wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu na ***watumishi*** **1,223** ya muda mfupi. Lengo ni kuwajengea uwezo na kuongeza weledi katika utekelezaji wa majukumu.

114.***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuwawezesha watumishi kufanya kazi katika mazingira bora kwa lengo la kuhakikisha wanakuwa na vitendea kazi katika utoaji wa huduma. Katika kufanikisha lengo hilo, hadi tarehe 15 Mei 2026, Wizara imenunua magari saba (**7**) kwa ajili ya kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma. Aidha, ukarabati wa jengo la Ofisi ya Ardhi Mkoa wa Dar es Salaam awamu ya kwanza umekamilika. Vilevile, ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Wizara lenye uwezo wa kuhudumia watumishi zaidi ya **350** umekamilika na kuanza kutumika rasmi mwezi Julai, 2025.



*Jengo la Makao Makuu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi lililopo eneo la Mtumba jijini Dodoma*

115.***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuweka mikakati ya kuimarisha utendaji wenye tija na ufanisi wa huduma kwa wananchi kwa kutoa elimu kwa watumishi kuhusu umuhimu wa kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya utumishi wa umma katika kutekeleza majukumu yao. Aidha, Wizara imeendelea kuhimiza watumishi kuwajibika ipasavyo na kwa wakati, kusimamia matumizi sahihi ya mifumo ya usimamizi wa Ardhi, upimaji utendaji kazi kwa watumishi wa umma (e- Utendaji), Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (e-Watumishi), Mfumo wa barua

pepe za Serikali (GMS), Mfumo wa Utunzaji wa kumbukumbu wa Ofisi Mtandao (e-Office), Mfumo wa kupokea mrejesho kutoka kwa wananchi (e-Mrejesho), Mfumo wa kutathmini mahitaji ya watumishi wa e-Msawazo (HR-Assessment) na matumizi ya Kituo cha Huduma kwa Wateja.

116. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuchukua hatua za kinidhamu kwa watumishi wanaothibitika kufanya makosa au kutekeleza majukumu yao kinyume na Sheria na taratibu zilizopo ambapo hatua za awali za kinidhamu zimechukuliwa dhidi ya watumishi watano (**5**) waliotuhumiwa kukiuka maadili, weledi, sheria na kanuni za utumishi wa umma na kukutwa na tuhuma za kusababisha migogoro ya ardhi. Kamati za uchunguzi mbili (**2**) zimeundwa ili kuchunguza tuhuma hizo kwa mujibu wa kanuni ya 36 ya Kanuni za Utumishi wa Umma za Mwaka 2022, ili kuchukua hatua za kinidhamu kwa mujibu wa kanuni ya 42 ya Kanuni za Utumishi wa Umma za Mwaka 2022. **Nawaelekeza watumishi wote wa sekta ya ardhi kutimiza wajibu wao kwa kuzingatia utu na maadili ya utumishi wa umma katika kuwahudumia wananchi kikamilifu kwa mujibu wa sheria, kanuni, taratibu na miongozo iliyopo. Wizara haitamvumilia mtumishi yeyote atakayekiuka maadili ya kazi kwa kukwamisha nia na dhamira njema ya Mheshimiwa Dkt. Samia**

**Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kutoa huduma bora za ardhi kwa Watanzania.**

117. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/27, Wizara itaendelea kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi pamoja na kuwekea mkazo katika uwajibikaji, usimamizi wa misingi ya uadilifu na weledi katika utoaji wa huduma bora za ardhi nchini. Aidha, Wizara imepanga kuajiri watumishi **460**, kupandisha vyeo watumishi **672** na kubadilisha kada watumishi **13**. Aidha, Wizara itawawezesha watumishi **1,272** kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu wakiwemo watumishi **460** wa ajira mpya.

## HABARI NA ELIMU KWA UMMA

118. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Wizara na Taasisi zake imeendelea kutekeleza majukumu ya kutoa elimu kwa umma kupitia vipindi mbalimbali vya redio na televisheni, majarida, tovuti na mitandao ya kijamii kwa lengo la kuongeza uelewa, ushiriki na upatikanaji wa huduma za sekta ya ardhi kwa wananchi. Hadi tarehe 15 Mei 2026, Wizara imeshiriki Maonesho ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (Sabasaba), Maonesho ya Kilimo ya Nanenane pamoja na Maadhimisho ya Wiki ya Huduma za Kifedha. Aidha, kupitia kipindi cha televisheni cha

**“Maisha ni Nyumba”** kinachorushwa kupitia kituo cha ITV, jumla ya vipindi **52** vimeandaliwa na kurushwa. Wizara imeshiriki katika vipindi **183** vya televisheni mbalimbali nchini pamoja na vipindi **428** vya redio. Aidha, machapisho **16,218** yaliandaliwa na kusambazwa ambapo jumla ya wananchi **14,310,111** wamefikiwa.

119.***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendesha kampeni maalum ya kutoa elimu kwa wanawake kuhusu masuala ya umiliki wa ardhi ijulikanayo kama Samia Ardhi Kliniki iliyoongozwa na kaulimbiu isemayo ***“Mwanamke, Haki Yako, Miliki Ardhi Sasa”***. Lengo lilikuwa kuongeza uelewa, hamasa na umiliki wa ardhi kwa wanawake. Kampeni hiyo ilifanyika katika mikoa yote ya Tanzania Bara kuelekea Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wanawake yanayoadhimishwa kila mwaka tarehe 8 Machi. Kupitia kampeni hiyo, wananchi **16,864** walihudumiwa.




*Bi. Lucy Kabyemera, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (katikati) akishuhudia mkazi wa Dar es Salaam akikabidhiwa Hati wakati wa Samia Ardhi Kliniki*

120. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha ushirikiano baina ya Wizara na wadau katika utoaji wa huduma za ardhi, katika mwaka 2026/27 Wizara itaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu sekta ya ardhi kupitia vipindi mbalimbali vya redio na televisheni, majarida, tovuti, mitandao ya kijamii pamoja na maonesho ya Kitaifa na Kimataifa. Aidha, Wizara itaandaa semina kwa watu **100** wenye mahitaji maalum;

Kampeni mbili (**2**) za kuhamasisha usalama wa milki za ardhi; mkutano na wahariri wa vyombo vya habari; kusambaza jumbe fupi za maandishi (SMS); na kusambaza vipeperushi **62,150** kupitia makongamano na kampeni.

## USHIRIKI WA SEKTA BINAFSI

121. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara yangu imekuwa ikishirikiana na sekta binafsi katika kutekeleza majukumu ya sekta ya ardhi katika upangaji miji, urasimishaji makazi, upimaji, uthamini na uendelezaji milki. Ushiriki wa sekta binafsi umewezesha urasimishaji kwenye mitaa mbalimbali nchini yenye makazi yasiyopangwa, uthamini wa kawaida wa mali, uratibu na usimamizi wa shughuli za uwakala. Aidha, sekta hii imeendelea kushiriki katika maboresho ya sera, sheria na kanuni mbalimbali na kutoa maoni kuhusu namna bora ya kusimamia sekta ya ardhi.

122. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kutumia fursa hii kuwashukuru wadau wote kutoka sekta binafsi wakiwemo Chama cha Wapima Ardhi Tanzania (IST), Chama cha Wataalam wa Mipangomiji Tanzania, Chama cha Wataalam wa Milki Tanzania (AREPTA), Chama cha Wanasheria Tanzania (TLS), Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGOs) na Asasi za Kiraia (CBOs) kwa ushiriki wao katika kutekeleza majukumu ya sekta. Ushiriki wao katika upangaji, upimaji na uthamini wa mali; Kliniki

za Ardhi; na uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi umeongeza tija na ufanisi katika utoaji wa huduma za ardhi. Wizara inaahidi kuendelea kushirikiana na sekta binafsi katika utekelezaji wa majukumu ili kufikia malengo yaliyowekwa.

## SHUKRANI

123. ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee nawashukuru Mhandisi Anthony Damian Sanga, Katibu Mkuu; na Bi. Lucy Dominico Kabyemera, Naibu Katibu Mkuu kwa ushirikiano wao katika kutekeleza majukumu ya kusimamia sekta hii muhimu. Aidha, nawashukuru Bw. Nathaniel Mathew Nhonge, Kamishna wa Ardhi; Bi. Evelyne Baruti Mugasha, Mthamini Mkuu; Bi. Stella Chaggi Tullo, Msajili wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya; Bw. Hamad Abdallah Hamad, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Nyumba la Taifa; na Bw. Joseph Constantine Mafuru, Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi. Pia, nawashukuru Wakuu wa Idara na Vitengo, Wenyeviti wa Bodi; na watumishi wote wa Wizara na Taasisi kwa kutekeleza majukumu yao kwa juhudi na maarifa ili kufikia malengo ya Wizara.

124. ***Mheshimiwa Spika,*** natoa shukrani na pongezi za dhati kwa viongozi wa Chama Cha Mapinduzi katika ngazi zote kwa maelekezo, miongozo, ushauri na ushirikiano wanaoendelea kunipatia katika utekelezaji wa majukumu

yangu. Aidha, nawashukuru wananchi wa Jimbo la Masasi kwa ushirikiano mkubwa wanaoendelea kunipatia katika utekelezaji wa jukumu la kuwawakilisha Bungeni. Kwa namna ya pekee napenda kuishukuru familia yangu na hasa mke wangu Bi. Grace Akwilapo na watoto wangu Catherine Akwilapo, Felix Akwilapo na Emmanuel Akwilapo pamoja na wajukuu zangu kwa upendo, ushauri, uvumilivu na kunitia moyo wakati wote nikiwa katika utekelezaji wa majukumu yangu. Pia, nawashukuru viongozi wa dini kwa sala na dua ambazo zimeendelea kunipa nguvu katika kutekeleza majukumu niliyonayo.

125.***Mheshimiwa Spika,*** naomba nitumie fursa hii kuwashukuru Washirika wa Maendeleo ambao Serikali imekuwa ikishirikiana nao katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo zinazohusiana na Sekta ya Ardhi. Washirika hao ni pamoja na Benki ya EXIM ya Korea Kusini, UN-HABITAT, *Shelter Afrique, African Union Boarder Program, Regional Centre for Mapping of Resources for Development (RCMRD), Tanzania Mortgage Refinance Company (TMRC), Watumishi Housing Company,* Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), *Association for Development of Protected Areas* (ADAP), Taasisi za fedha za ndani, Asasi za Kiraia, Sekta Binafsi na wananchi kwa michango yao katika

utekelezaji wa majukumu ya sekta ya ardhi. Aidha, napenda kutoa shukrani kwa vyombo vya habari kwa ushirikiano mzuri waliotupatia katika kutoa elimu na hamasa kwa umma kuhusu masuala ya sekta ya ardhi. Kwa hakika, wanahabari wameiwezesha Wizara kuwafikia wadau wengi zaidi kwa namna mbalimbali.

## HITIMISHO

126. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuhitimisha hotuba yangu kwa kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara katika mwaka 2026/27, itaendelea kuimarisha uratibu na usimamizi wa maendeleo ya Sekta ya Ardhi kwa kuzingatia vipaumbele vilivyoainishwa katika Hotuba hii. Aidha, kwa mara nyingine nitumie fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa ushirikiano mnaoendelea kunipatia katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Pamoja na hotuba hii, yameambatishwa majedwali ambayo yanafafanua kwa kina shughuli zilizotekelezwa na Wizara. Hotuba hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Wizara ambayo ni *www.lands.go.tz*.

## MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2026/27

127. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuwezesha utekelezaji wa vipaumbele na Mpango wa Bajeti wa Wizara kwa mwaka 2026/27, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lijadili na kuidhinisha bajeti ya jumla ya **Shilingi Bilioni Mia Mbili na kumi, Milioni Mia Mbili Hamsini na Tisa, Mia Tano Kumi na Tano Elfu (Shilingi 210,259,515,000)** kwa ajili ya matumizi ya mafungu yote mawili (**Fungu 48** - Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi) na (**Fungu 03** - Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi) kwa mchanganuo ufuatao: -

i) **Shilingi Bilioni Mia Moja, Milioni Mia Mbili Ishirini na Nne, Mia Tano Hamsini na Tatu Elfu (Shilingi 100,224,553,000)** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi Bilioni Sitini na Moja, Milioni Mia Moja Thelathini na Nne, Mia Tano Hamsini Elfu (Shilingi 61,134,550,000)** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi (PE) wa Wizara na Tume na **Shilingi Bilioni Thelathini na Tisa, Milioni Tisini, na Tatu Elfu (Shilingi 39,090,003,000)** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC); na

ii) **Shilingi Bilioni Mia Moja na Kumi, Milioni Thelathini na Nne, Mia Tisa Sitini na Mbili Elfu (Shilingi 110,034,962,000)** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo,

Shilingi **Bilioni Arobaini na Nne, Milioni Mia Moja Thelathini na Mbili, Mia Nne Sitini na Tisa Elfu (Shilingi 44,132,469,000)** ni Fedha za Ndani na Shilingi **Bilioni Sitini na Tano, Milioni Mia Tisa na Mbili, Mia Nne Tisini na Tatu Elfu (Shilingi 65,902,493,000)** ni Fedha za Nje.

**Mchanganuo wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara (Fungu 48) na Tume (Fungu 03) kwa mwaka 2026/27**

| | **AINA YA MATUMIZI** | **FEDHA ZINAZOOMBWA** |
|---|---|---|
| A | **Mapato ya Serikali** | |
| | i) Fungu 48 | 300,000,000,000 |
| | ii) Fungu 03 | 18,000,000 |
| | **Jumla (A)** | **300,018,000,000** |
| | **MAKISIO YA MATUMIZI FEDHA ZINAZOOMBWA** | |
| B | **Matumizi ya Kawaida** | |
| | Mishahara (PE) - Fungu 48 | 56,711,082,000 |
| | Mishahara (PE) - Fungu 03 | 4,423,468,000 |
| | **Jumla ya Mishahara (PE)** | **61,134,550,000** |
| | OC – Fungu 48 | 33,803,211,000 |
| | OC – Fungu 03 | 5,286,792,000 |
| | **Jumla ya OC** | **39,090,003,000** |
| | **Jumla (B)** | **100,224,553,000** |
| C | **Matumizi ya Maendeleo** | |
| | Fedha za Ndani - Fungu 48 | 5,732,469,000 |
| | Fedha za Ndani - Fungu 03 | 38,400,000,000 |
| | **Jumla ya Fedha za Ndani** | **44,132,469,000** |
| | Fedha za Nje - Fungu 48 | 65,902,493,000 |
| | **Jumla (C)** | **110,034,962,000** |
| | **JUMLA KUU (B+C)** | **210,259,515,000** |

128. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

**Jedwali Na. 1: Mchanganuo wa Fedha za Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo zilizopokelewa na kutumika hadi tarehe 15 Mei, 2026 - Fungu 48**

| Aina ya Bajeti | | Kiasi Kilichoidhinishwa na uhamisho | Kiasi cha Fedha Kilichopokelewa | % ya Fedha Zilizopokelewa | Kiasi cha Fedha Kilichotumika | % ya Fedha Zilizotumika |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Matumizi ya Kawaida** | Mishahara (**PE**) | 53,820,915,000.00 | 43,847,918,632.10 | 81.47 | 43,839,983,528.10 | 99.82 |
| | Matumizi Mengine yo (**OC**) | 37,559,123,000.00 | 31,509,227,849.96 | 83.89 | 29,819,226,800.25 | 98.83 |
| **Jumla ya Matumizi ya Kawaida** | | **91,380,038,000.00** | **75,357,146,482.06** | **82.47** | **73,659,210,328.35** | **99.45** |
| **Miradi ya Maendeleo** | Ndani | 69,970,254,049.38 | 65,737,785,049.38 | 93.95 | 63,888,460,780.37 | 99.39 |
| | Nje | 56,325,360,000.00 | - | - | - | - |
| **Jumla ya Miradi ya Maendeleo** | | **126,295,614,049.38** | **65,737,785,049.38** | **52.05** | **63,888,460,780.37** | **98.62** |
| **JUMLA YA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO** | | **217,675,652,049.38** | **141,094,931,531.44** | **64.82** | **137,547,671,108.72** | **95.51** |

**Jedwali Na. 2: Mchanganuo wa Fedha za Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo Zilizopokelewa na Kutumika hadi tarehe 15 Mei, 2026 - Fungu 03**

| Aina ya Bajeti | | Kiasi Kilichoidhinishwa | Kiasi cha Fedha Kilichopokelewa | % ya Fedha Zilizopokelewa | Kiasi cha Fedha Kilichotumika | % ya Fedha Zilizotumika |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Matumizi ya kawaida** | Mishahara **(PE)** | 4,712,143,000 | 3,580,932,000.00 | 75.99 | 3,580,932,000.00 | 100 |
| | Matumizi Mengineyo **(OC)** | 3,475,426,000 | 2,232,259,041.68 | 64.23 | 2,231,932,184.46 | 99.98 |
| **Jumla ya Matumizi ya Kawaida** | | **8,187,569,000** | **5,813,191,041.68** | **61.96** | **5,812,864,184.46** | **97.72** |
| **Miradi ya Maendeleo** | | **4,520,616,000** | **4,520,616,000.00** | **100** | **4,430,035,033.28** | **98** |
| **JUMLA YA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO** | | **12,708,185,000** | **10,333,807,041.68** | **81.27** | **10,242,899,217.74** | **99.12** |

**Jedwali Na. 3: Idadi ya Hatimiliki, Hati za Hakimiliki ya Kimila, Hati za Sehemu ya Jengo, Vyeti vya Ardhi ya Kijiji na Miamala ya Hatimiliki na Nyaraka za Kisheria Katika Mikoa hadi tarehe 15 Mei, 2026**

| Na. | Mkoa | Hatimiliki | Hati za Hakimiliki ya Kimila | Hati za Sehemu ya Jengo | Vyeti vya Ardhi ya Kijiji | Miamala ya Hatimiliki na Nyaraka za Kisheria |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Arusha | 2,430 | 1,941 | - | - | 7,901 |
| 2. | Dar es Salaam | 21,153 | - | 891 | - | 57,657 |
| 3. | Dodoma | 21,951 | 1,539 | - | 4 | 9,044 |
| 4. | Geita | 2,911 | 12 | - | 1 | 1,538 |
| 5. | Iringa | 3,902 | 1633 | - | 21 | 2,625 |
| 6. | Kagera | 1,905 | 154 | - | - | 2,807 |
| 7. | Katavi | 1,953 | 1,902 | - | - | 689 |
| 8. | Kigoma | 1,466 | 876 | - | - | 1,666 |
| 9. | Kilimanjaro | 1,542 | 326 | - | - | 4,118 |
| 10. | Lindi | 1,636 | 4,610 | - | 4 | 1,020 |
| 11. | Manyara | 1,701 | 902 | - | 4 | 1,492 |
| 12. | Mara | 1,687 | 1,874 | - | - | 1,946 |
| 13. | Mbeya | 5,372 | 8,103 | - | 13 | 2,856 |
| 14. | Morogoro | 4,848 | 21,024 | - | - | 5,572 |
| 15. | Mtwara | 2,619 | 41 | - | 38 | 1,164 |
| 16. | Mwanza | 3,888 | 19,993 | - | - | 14,794 |
| 17. | Njombe | 2,908 | 601 | - | - | 1,514 |

| Na. | Mkoa | Hatimiliki | Hati za Hakimiliki ya Kimila | Hati za Sehemu ya Jengo | Vyeti vya Ardhi ya Kijiji | Miamala ya Hatimiliki na Nyaraka za Kisheria |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 18. | Pwani | 7,664 | 3,802 | - | 1 | 5,850 |
| 19. | Rukwa | 1,040 | 4945 | - | - | 845 |
| 20. | Ruvuma | 1,786 | 10,802 | - | 22 | 1,637 |
| 21. | Shinyanga | 3,381 | 2,822 | - | - | 2,377 |
| 22. | Simiyu | 1,155 | 2,400 | - | - | 891 |
| 23. | Singida | 1,493 | 4,964 | - | 4 | 775 |
| 24. | Songwe | 1,103 | 458 | - | - | 1,311 |
| 25. | Tabora | 2,442 | 2,345 | - | 32 | 1,531 |
| 26. | Tanga | 3,747 | 1693 | 23 | 4 | 4,061 |
| **JUMLA** | | **107,683** | **99,762** | **914** | **148** | **137,681** |

**Jedwali Na. 4: Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi Kimkoa hadi tarehe 15 Mei, 2026**

| Na. | Mkoa | Utatuzi Wa Migogoro Kiutawala | |
|---|---|---|---|
| | | Kliniki ya Ardhi | Njia za Kawaida |
| 1. | Arusha | - | 38 |
| 2. | Dar es Salaam | 1,982 | 88 |
| 3. | Dodoma | 1,020 | 87 |
| 4. | Geita | - | 53 |
| 5. | Iringa | - | 72 |
| 6. | Kagera | - | 79 |
| 7. | Katavi | - | 59 |
| 8. | Kigoma | - | 436 |
| 9. | Kilimanjaro | - | 73 |
| 10. | Lindi | - | 53 |
| 11. | Manyara | - | 55 |
| 12. | Mara | - | 79 |
| 13. | Mbeya | - | 182 |
| 14. | Morogoro | - | 50 |
| 15. | Mtwara | - | 70 |
| 16. | Mwanza | - | 51 |
| 17. | Njombe | - | 72 |
| 18. | Pwani | - | 175 |
| 19. | Rukwa | - | 31 |
| 20. | Ruvuma | - | 78 |
| 21. | Shinyanga | 181 | 83 |
| 22. | Simiyu | - | 17 |
| 23. | Singida | - | 79 |
| 24. | Songwe | - | 72 |
| 25. | Tabora | - | 161 |
| 26. | Tanga | - | 97 |
| **JUMLA** | | **3,183** | **2,390** |

**Jedwali Na. 5: Mchanganuo wa maeneo yaliyolipwa fidia katika Vijiji/Mitaa 975 hadi tarehe 15 Mei, 2026**

| Na. | Eneo | Vijiji/Mitaa | Kiasi |
|---|---|---|---|
| 1. | Hifadhi ya Taifa ya Saadani | Kaya 17 na mashamba 22 katika Kitongoji cha Uvinje | 376,436,839.60 |
| 2. | Hifadhi ya Taifa Arusha | Wananchi 15 ndani ya Shamba Na. 358 katika kijiji cha Orkung'wado | 135,365,800.00 |
| 3. | Hifadhi ya Maji - Mto THEMI | Wananchi 51 wa Kijiji cha Kivuluvulu na 42 wa Kijiji cha Olgilai | 887,043,462.00 |
| 4. | Hifadhi ya Bwawa la Farkwa | Wananchi wa vijiji vya Bubutole na Mombose | 8,519,354,498.72 |
| 5. | Hifadhi ya Maji Nyakanasi | Wananchi 6 wa Mtaa wa Nyakanasi | 73,146,200.56 |
| 6. | Eneo la Ghuba ya Speke | Tamau, Serengeti, Nyatwali na Kariakoo | 53,407,045,111.87 |
| 7. | Shamba la utegi | Kitongoji cha Kibinyongo, Mabatini, Oringa, Denga, Omuga na Shule ya Msingi Utengi | 7,727,036,577.31 |
| 8. | Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Kilimanjaro (KIA) | Kijiji cha Chemka, Mtakuja, Tindigani, Samaria Kati, Majengo, Mhula na Sanya Station | 11,321,898,061.00 |
| 9. | Pori la Akiba Mto Kilombero | Kijiji cha Ngombo | 6,946,514,040.00 |
| 10. | Pori la Akiba Mkungunero | Kaya **145** katika vitongoji vya Kagera, Msumbiji, Elbenek na Ndaja katika vijiji vya Kisondoko na Keikei | 482,567,678.48 |
| 11. | Hifadhi ya Taifa Mahale | Vitongoji vya Kabukuyungu na Mahasa | 1,681,882,027.00 |
| 12. | Bwawa la Milala | Mtaa wa Milala Mpanda | 2,946,954,048.15 |
| 13. | Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi | Kitongoji cha Kimuuni katika Kijiji cha Mkota | 711,592,221.00 |
| 14. | Hifadhi ya Msitu Mkuti | Kanisa la wasabato Rungwe mpya | 53,838,381.62 |
| **JUMLA** | | | **95,270,674,947.31** |

**Jedwali Na. 6: Viwanja/Mashamba Yaliyopimwa na Kuidhinishwa Hadi Tarehe 15 Mei, 2026**

| Na. | Mkoa | Idadi ya Viwanja | Idadi ya Mashamba |
|---|---|---|---|
| 1. | Arusha | 2,676 | - |
| 2. | Dar es salaam | 22,850 | - |
| 3. | Dodoma | 10,650 | - |
| 4. | Geita | 7,981 | 9 |
| 5. | Iringa | 15,516 | 17 |
| 6. | Kagera | 2,983 | 96 |
| 7. | Katavi | 3,317 | 35 |
| 8. | Kigoma | 2,904 | 22 |
| 9. | Kilimanjaro | 2,457 | - |
| 10. | Lindi | 6,635 | 8 |
| 11. | Manyara | 2735 | 3 |
| 12. | Mara | 1,790 | - |
| 13. | Mbeya | 20,674 | - |
| 14. | Morogoro | 8,724 | 113 |
| 15. | Mtwara | 2,816 | 4 |
| 16. | Mwanza | 3,589 | - |
| 17. | Njombe | 6,520 | - |
| 18. | Pwani | 28,439 | 116 |
| 19. | Rukwa | 1,966 | 19 |
| 20. | Ruvuma | 7,543 | 15 |
| 21. | Shinyanga | 4,412 | 6 |
| 22. | Simiyu | 914 | 3 |
| 23. | Singida | 9,895 | 43 |
| 24. | Songwe | 4,939 | 6 |
| 25. | Tabora | 3,394 | - |
| 26. | Tanga | 6,998 | - |
| **JUMLA** | | **193,317** | **515** |

**Jedwali Na. 7: Idadi ya Vijiji Vilivyopimwa Mipaka, Kuhakikiwa na Kuhuishwa hadi tarehe 15 Mei, 2026**

| Na. | MKOA | VIJIJI VILIVYOPIMWA | VIJIJI VILIVYOHAKIKIWA NA KUHUISHWA |
|---|---|---|---|
| 27. | Geita | 19 | - |
| 28. | Iringa | 9 | - |
| 29. | Kilimanjaro | 90 | - |
| 30. | Mtwara | 6 | 25 |
| 31. | Njombe | 0 | 3 |
| 32. | Shinyanga | 45 | - |
| 33. | Tabora | 10 | 14 |
| 34. | Tanga | 10 | 12 |
| **JUMLA** | | **189** | **54** |

**Jedwali Na. 8: Maeneo Yaliyoiva Kuendelezwa Kimji**

| Na. | Mkoa | Idadi ya Matangazo | Halmashauri | Tangazo |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Dar es Salaam | 2 | Kinondoni MC | Amri ya Uendelezaji Upya wa Eneo la Makangira - Msasani ya mwaka 2026 |
| | | | Temeke MC | Amri ya Uendelezaji Upya wa Eneo la Tandika ya mwaka 2026 |
| 2. | Manyara | 1 | Mbulu TC | Amri ya Kuandaa Mpango wa Jumla wa Mji Mbulu ya mwaka 2026 |
| 3. | Ruvuma | 1 | Mbinga TC | Amri ya Kuandaa Mpango wa Jumla wa Mji Mbinga ya mwaka 2026 |
| 4. | Njombe | 6 | Njombe TC | Amri ya Kuandaa Mpango wa Jumla wa Mji Makambako ya mwaka 2026 |
| | | | Ludewa DC | Amri ya Kurasimisha Makazi Yasiyopangwa Eneo la Nsungu ya mwaka 2026. |
| | | | | Amri ya Kurasimisha Makazi Yasiyopangwa Eneo la Luilo ya mwaka 2026. |
| | | | | Amri ya Kurasimisha Makazi Yasiyopangwa Eneo la Mawengi ya mwaka 2026. |
| | | | | Amri ya Kurasimisha Makazi Yasiyopangwa Eneo la Mkiu ya mwaka 2026. |
| | | | Wanging'ombe DC | Amri ya Kupanga Eneo la Lusisi ya mwaka 2026. |
| 5. | Morogoro | 1 | Kilombero DC | Amri ya Kuandaa Mpango wa Jumla wa Mji Ifakara ya mwaka 2026. |
| 6. | Kigoma | 1 | Kasulu TC | Amri ya Kuandaa Mpango wa Jumla wa Mji Kasulu ya mwaka 2026. |

| Na. | Mkoa | Idadi ya Matangazo | Halmashauri | Tangazo |
|---|---|---|---|---|
| 7. | Geita | 2 | Chato DC | Amri ya Kuandaa Mpango wa Jumla wa Wilaya ya Chato ya mwaka 2026. |
| | | | Geita DC | Amri ya Kupanga Eneo la Ngula ya mwaka 2026 |
| 8. | Songwe | 6 | Mbozi DC | Amri ya Kuandaa Mpango wa Jumla wa Wilaya ya Mbozi ya mwaka 2026 |
| | | | Ileje DC | Amri ya Kupanga Eneo la Malale ya mwaka 2026. |
| | | | | Amri ya Kupanga Eneo la Mbebe na Mapogoro ya mwaka 2026. |
| | | | | Amri ya Kupanga Eneo la Ikumbilo na Msia ya mwaka 2026. |
| | | | | Amri ya Kupanga Eneo la Izuba ya mwaka 2026. |
| | | | | Amri ya Kupanga Eneo la Ilulu ya mwaka 2026. |
| 9. | Mtwara | 3 | Masasi | Amri ya Kuandaa Mpango wa Jumla wa Mji Masasi ya mwaka 2026 |
| | | | Newala | Amri ya Kuandaa Mpango wa Jumla wa Mji Newala ya mwaka 2026 |
| | | | Nanyamba TC | Amri ya Kuandaa Mpango wa Jumla wa Mji Nanyamba ya mwaka 2026 |
| 10. | Lindi | 2 | Ruangwa DC | Amri ya Kupanga Eneo la Ng'au ya mwaka 2026. |
| | | | | Amri ya Kupanga Eneo la Namungo ya mwaka 2026. |

| Na. | Mkoa | Idadi ya Matangazo | Halmashauri | Tangazo |
|---|---|---|---|---|
| | | 1 | Kilwa DC | Amri ya kupanga Eneo la Mtoni ya Mwaka 2026 |
| 11. | Mara | 2 | Tarime TC | Amri ya Kuandaa Mpango wa Jumla wa Mji Tarime ya mwaka 2026 |
| | | | Bunda TC | Amri ya Kuandaa Mpango wa Jumla wa Mji Bunda ya mwaka 2026 |
| 12. | Dodoma | 1 | Kondoa TC | Amri ya Kuandaa Mpango wa Jumla wa Mji Kondoa ya mwaka 2026 |
| 13. | Tabora | 1 | Nzega TC | Amri ya Kuandaa Mpango wa Jumla wa Mji Nzega ya mwaka 2026 |
| 14. | Tanga | 5 | Handeni TC | Amri ya Kuandaa Mpango wa Jumla wa Mji Handeni ya mwaka 2026 |
| | | | | Amri ya kupanga eneo la Chogo ya mwaka 2026. |
| | | | | Amri ya kupanga eneo la Mkalamo - Kwamsisi ya mwaka 2026. |
| | | | Muheza DC | Amri ya Upangaji Maalum eneo la Bwitini ya mwaka 2026. |
| | | | Mkinga DC | Amri ya Kupanga Eneo la Mapatano, Mbuyuni na Mwanyumba ya mwaka 2026. |
| 15. | Pwani | 1 | Mkuranga DC | Amri ya Kuandaa Mpango wa Jumla wa Wilaya ya Mkuranga ya mwaka 2026 |
| 16. | Iringa | 2 | Kilolo DC | Amri ya Kupanga Eneo la Lugalo ya mwaka 2026. |
| | | | | Amri ya Kupanga Eneo la Mbigili ya mwaka 2026. |

| Na. | Mkoa | Idadi ya Matangazo | Halmashauri | Tangazo |
|---|---|---|---|---|
| 17. | Rukwa | 3 | Kalambo DC | Amri ya Kupanga Eneo la Malale ya mwaka, 2026. |
| | | | | Amri ya Kupanga Eneo la Mbebe na Mapogoro ya mwaka 2026. |
| | | | | Amri ya Kupanga Eneo la Ikumbilo na Msia ya mwaka 2026. |
| 18. | Shinyanga | 1 | Shinyanga DC | Amri ya Mpango Maalum wa Eneo la Bubale ya mwaka 2026. |
| **JUMLA** | | **42** | | |

**Jedwali Na.9: Orodha ya Halmashauri za Kundi la Tatu la Utekelezaji wa Mradi wa Tanzania Cities Transforming Infrastructure and Competitiveness (TACTIC) - Miji Itakayoandaliwa Mipango Kabambe**

| Na. | Halmashauri ya Mji | Mkoa |
|---|---|---|
| 1. | Bunda | Mara |
| 2. | Chato | Geita |
| 3. | Handeni | Tanga |
| 4. | Ifakara | Morogoro |
| 5. | Kasulu | Kigoma |
| 6. | Kondoa | Dodoma |
| 7. | Mafinga | Iringa |
| 8. | Makambako | Njombe |
| 9. | Masasi | Mtwara |
| 10. | Mbinga | Ruvuma |
| 11. | Mbulu | Manyara |
| 12. | Nanyamba | Mtwara |
| 13. | Newala | Mtwara |
| 14. | Nzega | Tabora |
| 15. | Rufiji | Pwani |
| 16. | Tarime | Mara |
| 17. | Tunduma | Songwe |
| 18. | Vwawa | Songwe |

**Jedwali Na.10: Taarifa ya Uandaaji Mipangokina Kimkoa Hadi Tarehe 15 Mei, 2026**

| Na. | Mkoa | Idadi ya Michoro (TPs) | Idadi ya Viwanja Kwenye Michoro (TPs) |
|---|---|---|---|
| 1. | Arusha | 321 | 14,020 |
| 2. | Dar es Salaam | 862 | 32,131 |
| 3. | Dodoma | 139 | 10,280 |
| 4. | Geita | 103 | 9,751 |
| 5. | Iringa | 139 | 11,592 |
| 6. | Kagera | 99 | 3,429 |
| 7. | Katavi | 19 | 6,396 |
| 8. | Kigoma | 35 | 5,811 |
| 9. | Kilimanjaro | 82 | 5,446 |
| 10. | Lindi | 70 | 11,888 |
| 11. | Manyara | 40 | 1,120 |
| 12. | Mara | 68 | 4,523 |
| 13. | Mbeya | 13 | 3,243 |
| 14. | Morogoro | 151 | 10,454 |
| 15. | Mtwara | 25 | 1,590 |
| 16. | Mwanza | 143 | 21,717 |
| 17. | Njombe | 76 | 10,336 |
| 18. | Pwani | 798 | 77,251 |
| 19. | Rukwa | 30 | 3,169 |
| 20. | Ruvuma | 52 | 10,751 |
| 21. | Shinyanga | 116 | 12,946 |
| 22. | Simiyu | 28 | 4,805 |
| 23. | Singida | 74 | 9,537 |
| 24. | Songwe | 69 | 11,081 |
| 25. | Tabora | 47 | 11,482 |
| 26. | Tanga | 96 | 10,538 |
| **JUMLA** | | **3,695** | **315,287** |

**Jedwali Na. 11: Urasimishaji Makazi Nchini hadi tarehe 15 Mei, 2026**

| Na. | Mkoa | Makazi yaliyorasimishwa |
|---|---|---|
| 1. | Arusha | 1,753 |
| 2. | Dar es Salaam | 10,747 |
| 3. | Dodoma | - |
| 4. | Geita | 20,045 |
| 5. | Iringa | 19,896 |
| 6. | Kagera | 2,676 |
| 7. | Katavi | 971 |
| 8. | Kigoma | 3,595 |
| 9. | Kilimanjaro | 3,851 |
| 10. | Lindi | 10,349 |
| 11. | Manyara | 240 |
| 12. | Mara | 2,391 |
| 13. | Mbeya | 21,453 |
| 14. | Morogoro | 1,443 |
| 15. | Mtwara | 1,164 |
| 16. | Mwanza | 3,851 |
| 17. | Njombe | 17,153 |
| 18. | Pwani | 9,284 |
| 19. | Rukwa | 799 |
| 20. | Ruvuma | 1,263 |
| 21. | Shinyanga | 5,260 |
| 22. | Simiyu | 2,441 |
| 23. | Singida | 2,149 |
| 24. | Songwe | 1,880 |
| 25. | Tabora | 5,130 |
| 26. | Tanga | - |
| **JUMLA** | | **149,784** |

**Jedwali Na. 12: Orodha ya Maeneo Chakavu Yaliyoainishwa Kwa Ajili ya Uendelezaji Upya na Uboreshaji wa Miji**

| Na. | Mkoa | Halmashauri | Eneo | Ukubwa (Ha) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Katavi | Mpanda MC | Msasani | 347 |
| | | | Uwanja wa ndege | 269 |
| | | | Ikulu | 197 |
| | | | **Jumla** | **813** |
| 2. | Shinyanga | Shinyanga MC | Kambarage | 615 |
| | | | Shinyanga Mjini | 150 |
| | | | Ngokolo | 753 |
| | | Kahama MC | Nyahanga | 1824 |
| | | | Kahama mjini | 142.7 |
| | | | Nyasubi | 652 |
| | | | Nyihogo | 119 |
| | | | Malunga | 1083 |
| | | | **Jumla** | **5,338.7** |
| 3. | Lindi | Lindi MC | Mitwero Stand | 150 |
| | | | Mmongo | 122 |
| | | | Mnazi | 98 |
| | | Nachingwea DC | Majengo | 6.82 |
| | | | Uhindini | 12.35 |
| | | | **Jumla** | **389.17** |
| 4. | Kilimanjaro | Moshi MC | Rauya | 90 |
| | | | Msufini | 204 |
| | | | Saranga | 144 |
| | | | **Jumla** | **438** |

| Na. | Mkoa | Halmashauri | Eneo | Ukubwa (Ha) |
|---|---|---|---|---|
| 5. | Mwanza | Mwanza CC | Igogo | 38.95 |
| | | | Bugarika | 88.59 |
| | | | Mabatini | 78.82 |
| | | | **Jumla** | **206.36** |
| 6. | Geita | Geita TC | Nyerere | 33.72 |
| | | | Kivukoni | 42.42 |
| | | | Msalala | 103.38 |
| | | | **Jumla** | **179.52** |
| 7. | Manyara | Babati TC | Gendi | 375 |
| | | | Maisaka Kati | 407 |
| | | | Mruki/Sinai | 291 |
| | | | **Jumla** | **1,073** |
| 8. | Ruvuma | Songea MC | Bombambili (Merikebu) | 74.08 |
| | | | Lizaboni | 314.49 |
| | | | Ruvuma chini | 269.57 |
| | | | **Jumla** | **658.14** |
| 9. | Kagera | Bukoba MC | Buhembe | 264.6 |
| | | | Kahororo | 43.3 |
| | | | Omukigusha | 15.4 |
| | | | **Jumla** | **323.3** |
| 10. | Songwe | Tunduma TC | Tukuyu | 48 |
| | | Mbozi DC | Mlowo | 47 |
| | | | Mlowo kati | 56 |
| | | | **Jumla** | **151** |
| 11. | Morogoro | Morogoro MC | Genda | 10 |
| | | | Mkwajuni | 7 |

| Na. | Mkoa | Halmashauri | Eneo | Ukubwa (Ha) |
|---|---|---|---|---|
| | | | Mwigole | 10 |
| | | | Ndegewengi | 6 |
| | | | Mtawala | 8 |
| | | | Gohalema | 10 |
| | | | **Jumla** | **51** |
| 12. | Mtwara | Mtwara Mikindani MC | Mdenga | 140 |
| | | | Chiputa | 120 |
| | | Masasi TC | Mkuti Kati | 70 |
| | | | Mkunguni | 50 |
| | | | Wapiwapi | 50 |
| | | | Kisiwani | 30 |
| | | | **Jumla** | **460** |
| 13. | Njombe | Njombe TC | Njombe Mjini | 500 |
| | | Makambako TC | Ndondole | 100 |
| | | | Mkulima | 100 |
| | | | Mangula | 100 |
| | | | Lumumba | 100 |
| | | | **Jumla** | **900** |
| 14. | Tabora | Tabora MC | Ng'ambo | 18 |
| | | | Chemchem | 18.5 |
| | | | **Jumla** | **36.5** |
| 15. | Mara | Musoma MC | Nyakato Mlimani | 55 |
| | | | Mshikamano saanane | 75 |
| | | | Kigera | 40 |
| | | | **Jumla** | **170** |
| 16. | Singida | Singida MC | Manguanjuki | 101 |
| | | | Karakana | 95 |

| Na. | Mkoa | Halmashauri | Eneo | Ukubwa (Ha) |
|---|---|---|---|---|
| | | | Muhawa | 114 |
| | | | **Jumla** | **310** |
| 17. | Kigoma | Kigoma Ujiji MC | Rubuga | 67.06 |
| | | | Mwenge | 26.6 |
| | | | Kitangoni | 121.35 |
| | | | Mwanga | 60 |
| | | | Majengo | 102 |
| | | | **Jumla** | **377.01** |
| 18. | Arusha | Arusha CC | Unga Ltd | 43 |
| | | | Ngarenaro | 23 |
| | | | Kiranyi | 33 |
| | | | Moivo | 70 |
| | | | **Jumla** | **169** |
| 19. | Pwani | Kibaha MC | Mailimoja | 568 |
| | | | Picha ya ndege | 122 |
| | | Kibaha DC | Mlandizi | 319 |
| | | Mkuranga DC | Kiparampakani | 1026 |
| | | | **Jumla** | **2035** |
| 20. | Dar es Salaam | Kinondoni MC | Bonde la Mpunga | 79 |
| | | | Makangira, | 95.2 |
| | | | Mikoroshoni | 102 |
| | | | Mikocheni B | 78.792 |
| | | | Manzese Uzuri | 1,729.159 |
| | | | Kinondoni Shamba | 78.83 |
| | | | Namanga- Msasani | 226.2 |
| | | | Kawe | 3,081.28 |
| | | | Kinondoni area | 89.7 |

| Na. | Mkoa | Halmashauri | Eneo | Ukubwa (Ha) |
|---|---|---|---|---|
| | | | Kijitonyama | 103.2 |
| | | | Mbezi Beach (Block BC) | 47.8 |
| | | | Mbezi Kawe | 79.4 |
| | | | Mikocheni A (Eneo la makaburi) | 105.591 |
| | | | **Jumla** | **5,473.772** |
| | | Ubungo MC | Ubungo Kisiwani | 23.45 |
| | | | Manzese Uzuri | 105.78 |
| | | | Mbezi Mwisho | 246.6 |
| | | | Mabibo | 88.4 |
| | | | **Jumla** | **464.23** |
| | | Temeke MC | Mtoni Kijichi | 48.6 |
| | | | **Jumla** | **48.6** |
| | | Ilala CC | Uwanja wa Ndege | 52.66 |
| | | | Kipawa Industrial | 49.6 |
| | | | Mabibo na Kigogo | 1677.74 |
| | | | Keko | 284.663 |
| | | | Buguruni | 101.784 |
| | | | Kiwalani | 32.5 |
| | | | **Jumla** | **2,198.447** |
| 21. | Mbeya | Mbeya CC | Maanga | 43.78 |
| | | | Ruanda | 130.26 |
| | | | Sinde | 54.88 |
| | | | **Jumla** | **228.92** |
| 22. | Iringa | Iringa MC | Gangilonga | 212.4 |
| | | | Kitanzini | 25.6 |

| Na. | Mkoa | Halmashauri | Eneo | Ukubwa (Ha) |
|---|---|---|---|---|
| | | | Mshindo | 13.2 |
| | | | Mlandege | 49.2 |
| | | | Makorongoni | 31.6 |
| | | | Ilala | 20.8 |
| | | | Kwa Kilosa | 34.4 |
| | | | Mivinjeni | 10.8 |
| | | | **Jumla** | **398** |
| 23. | Tanga | Tanga CC | Mwambani | 102 |
| | | | Ngamiani | 54 |
| | | | Kange Industrial | 70 |
| | | | **Jumla** | **271** |
| 24. | Simiyu | Bariadi CC | Bariadi Centre | 50.2 |
| | | | **Jumla** | **50.2** |
| 25. | Rukwa | Sumbawanga MC | Utengule | 325 |
| | | | Senti | 246 |
| | | | Isesa | 425 |
| | | | **Jumla** | **996** |
| **JUMLA KUU** | | | | **24,309.35** |

**Jedwali Na.13: Mikopo ya Ujenzi wa Nyumba Iliyotolewa na Benki**

| Na. | Benki Iliyotoa Mkopo | Idadi ya Akaunti Zilizokopeshwa | Kiasi (Bilioni) |
|---|---|---|---|
| 1. | CRDB BANK PLC | 1,655 | 225.13 |
| 2. | NMB BANK PLC | 762 | 91.83 |
| 3. | AZANIA BANK PUBLIC LIMITED COMPANY | 472 | 58.32 |
| 4. | TANZANIA COMMERCIAL BANK PLC | 425 | 37.59 |
| 5. | FIRST HOUSING FINANCE COMPANY LIMITED | 308 | 37.14 |
| 6. | STANBIC BANK TANZANIA LIMITED | 170 | 34.98 |
| 7. | DCB COMMERCIAL BANK PLC | 236 | 34.48 |
| 8. | KCB BANK TANZANIA LIMITED | 171 | 30.19 |
| 9. | EXIM BANK TANZANIA LIMITED | 196 | 29.07 |
| 10. | NATIONAL BANK OF COMMERCE LIMITED | 163 | 27.30 |
| 11. | ABSA BANK TANZANIA LIMITED | 123 | 25.06 |
| 12. | BANK OF AFRICA TANZANIA LIMITED | 86 | 14.53 |
| 13. | EQUITY BANK TANZANIA LIMITED | 94 | 11.25 |
| 14. | NCBA BANK TANZANIA LIMITED | 55 | 10.69 |
| 15. | ACCESS BANK TANZANIA LIMITED | 82 | 10.18 |
| 16. | AMANA BANK LIMITED | 135 | 9.33 |
| 17. | DIAMOND TRUST BANK TANZANIA PLC | 40 | 8.39 |

| Na. | Benki Iliyotoa Mkopo | Idadi ya Akaunti Zilizokopeshwa | Kiasi (Bilioni) |
|---|---|---|---|
| 18. | I & M BANK TANZANIA LIMITED | 36 | 5.92 |
| 19. | AKIBA COMMERCIAL BANK PLC | 40 | 3.38 |
| 20. | PEOPLES BANK OF ZANZIBAR LIMITED | 5 | 3.17 |
| 21. | ECOBANK TANZANIA LIMITED | 18 | 2.38 |
| 22. | MWANGA HAKIKA BANK LIMITED | 24 | 2.35 |
| 23. | MAENDELEO BANK PLC | 434 | 2.30 |
| 24. | BANK OF BARODA TANZANIA LIMITED | 18 | 1.76 |
| 25. | MUCOBA BANK PLC | 27 | 1.56 |
| 26. | MKOMBOZI COMMERCIAL BANK PLC | 10 | 1.02 |
| 27. | LETSHEGO FAIDIKA BANK TANZANIA LIMITED | 9 | 0.70 |
| 28. | TIB DEVELOPMENT BANK LIMITED | 8 | 0.67 |
| 29. | INTERNATIONAL COMMERCIAL BANK TANZANIA LIMITED | 3 | 0.13 |
| **JUMLA** | | **5,805** | **720.81** |

**Jedwali Na. 14: Taarifa ya Halmashauri Zilizokopeshwa Fedha Kwa Ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi (KKK) Mwaka 2021/22**

**(i) Halmashauri Zilizokamilisha Marejesho**

| Na. | Halmashauri | Mkopo | Marejesho |
|---|---|---|---|
| 1. | Moshi DC | 233,200,000 | 233,200,000 |
| 2. | Mwanza CC | 800,000,000 | 800,000,000 |
| 3. | Meru DC | 1,655,000,000 | 1,655,000,000 |
| 4. | Morogoro MC | 1,000,000,000 | 1,000,000,000 |
| 5. | Kilosa DC | 250,000,000 | 250,000,000 |
| 6. | Geita DC | 600,000,000 | 600,000,000 |
| 7. | Bariadi TC | 79,750,000 | 79,750,000 |
| 8. | Mbozi DC | 495,000,000 | 495,000,000 |
| 9. | Ilemela MC | 3,589,774,000 | 3,589,774,000 |
| 10. | Ileje DC | 432,319,000 | 432,319,000 |
| 11. | Tunduma TC | 543,000,000 | 543,000,000 |
| 12. | Songwe DC | 450,000,000 | 450,000,000 |
| 13. | Kaliua DC | 100,000,000 | 100,000,000 |
| 14. | Ofisi ya Ardhi Mkoa wa Iringa | 450,000,000 | 718,276,664 |
| 15. | Kigamboni MC | 1,500,000,000 | 1,500,000,000 |
| 16. | Kibaha TC | 1,588,000,000 | 1,588,000,000 |
| 17. | Sumbawanga DC | 47,630,000 | 47,630,000 |
| 18. | Mbulu DC | 162,500,000 | 162,500,000 |
| 19. | Tanga CC | 400,000,000 | 400,000,000 |

| Na. | Halmashauri | Mkopo | Marejesho |
|---|---|---|---|
| 20. | Hanang' DC | 187,500,000 | 187,500,000 |
| 21. | Rhombo DC | 1,060,000,000 | 1,060,000,000 |
| 22. | Njombe TC | 700,000,000 | 700,000,000 |
| 23. | Ushetu DC | 259,850,000 | 259,850,000 |
| 24. | Makambako TC | 683,300,000 | 683,300,000 |
| 25. | Dodoma CC | 3,000,000,000 | 3,000,000,000 |
| 26. | Chuo Kikuu Ardhi | 892,000,000 | 892,000,000 |
| 27. | Mbeya CC | 2,000,000,000 | 2,000,000,000 |
| **JUMLA** | | **23,158,823,000** | **23,427,099,664** |

**(ii) Halmashauri Zilizorejesha Sehemu ya Fedha**

| Na. | Halmashauri | Mkopo | Fedha zilizorejeshwa | Kiasi ambacho hakijarejeshwa | Asilimia |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Bunda TC | 493,989,000 | 472,830,000 | 21,159,000 | 96 |
| 2. | Mbeya DC | 584,000,000 | 480,000,000 | 104,000,000 | 82 |
| 3. | Buchosa DC | 327,000,000 | 261,000,000 | 66,000,000 | 80 |
| 4. | Uyui DC | 100,000,000 | 80,260,000 | 19,740,000 | 80 |
| 5. | Mtwara MC | 1,679,450,000 | 1,000,000,000 | 679,450,000 | 60 |
| 6. | Babati DC | 125,000,000 | 72,000,000 | 53,000,000 | 58 |
| 7. | Musoma MC | 250,000,000 | 136,391,000 | 113,609,000 | 55 |
| 8. | Chalinze DC | 2,500,000,000 | 1,766,583,655 | 733,416,345 | 71 |
| 9. | Mbinga TC | 330,000,000 | 167,130,984 | 162,869,016 | 51 |
| 10. | Butiama DC | 297,000,000 | 164,523,500 | 132,476,500 | 55 |
| 11. | Meatu DC | 93,500,000 | 45,000,000 | 48,500,000 | 48 |
| 12. | Tabora MC | 885,000,000 | 360,726,252 | 524,273,748 | 41 |
| 13. | Babati TC | 250,000,000 | 123,717,091 | 126,282,909 | 49 |
| 14. | Musoma DC | 200,000,000 | 80,000,000 | 120,000,000 | 40 |
| 15. | Tarime TC | 560,000,000 | 216,355,000 | 343,645,000 | 39 |
| 16. | Morogoro DC | 865,210,000 | 310,000,000 | 555,210,000 | 36 |
| 17. | Ludewa DC | 405,000,000 | 147,647,000 | 257,353,000 | 36 |
| 18. | Ikungi DC | 598,226,000 | 131,000,000 | 467,226,000 | 32 |
| 19. | Kishapu DC | 882,000,000 | 248,139,833 | 633,860,167 | 28 |
| 20. | Msalala DC | 1,609,500,000 | 441,171,000 | 1,168,329,000 | 27 |
| 21. | Rorya DC | 1,000,000,000 | 190,000,000 | 810,000,000 | 19 |

| Na. | Halmashauri | Mkopo | Fedha zilizorejeshwa | Kiasi ambacho hakijarejeshwa | Asilimia |
|---|---|---|---|---|---|
| 22. | Shinyanga DC | 900,000,000 | 225,468,858 | 674,531,142 | 25 |
| 23. | Maswa DC | 850,000,000 | 140,000,000 | 710,000,000 | 16 |
| 24. | Lushoto DC | 208,000,000 | 29,305,281 | 178,694,719 | 14 |
| 25. | Lindi MC | 1,600,000,000 | 211,530,000 | 1,388,470,000 | 13 |
| 26. | Chamwino DC | 300,000,000 | 40,000,000 | 260,000,000 | 13 |
| 27. | Mbulu TC | 455,000,000 | 50,000,000 | 405,000,000 | 15 |
| 28. | Shinyanga MC | 1,055,000,000 | 108,397,366 | 946,602,634 | 10 |
| 29. | Manyoni DC | 1,520,770,000 | 141,000,000 | 1,379,770,000 | 9 |
| 30. | Korogwe TC | 80,000,000 | 5,075,000 | 74,925,000 | 6 |
| 31. | Korogwe DC | 240,000,000 | 12,880,000 | 227,120,000 | 6 |
| **JUMLA** | | **21,243,645,000** | **7,858,131,820** | **13,385,513,180** | **63** |

**(iii) Hali ya Urejeshaji wa Fedha kutoka kwenye Vyuo vya Ardhi**

| Na. | Halmashauri | Mkopo | Fedha Zilizorejeshwa | Kiasi Ambacho Hakijarejeshwa | Asilimia za Urejeshaji |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | ARIMO | 1,273,038,500 | 250,000,000 | 1,023,038,500 | 20 |
| 2. | ARITA | 644,590,300 | 100,000,000 | 544,590,300 | 16 |
| **JUMLA** | | **1,917,628,800** | **350,000,000** | **1,567,628,800** | 18 |

**Jedwali Na. 15: Orodha ya Vijiji Vilivyoandaliwa Mipango ya Matumizi ya Ardhi hadi Tarehe 15 Mei, 2026.**

| Na. | Mkoa | H/Wilaya | Kijiji | Idadi |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Geita | Mbogwe | Budoda, Ng'homolwa, Nyanhwiga, Maguta, Nhungwiza, Mpakali, Nanda, Busambilo, Nsango, Nyashimba, Kabanga, Kanegere Bukandwe, Lubeho, Ikobe na Mtakuja | 16 |
| | | Nyang'wale | Isonda, Mimbili, Nyugwa, Lyulu, Nyangalamila, Igeka, Kijinga, Nundu na Nyang'holongo | 9 |
| 2. | Mtwara | Mtwara | Mnaida, Tangazo, Kilambo, Magomeni, Kihimika, Kitunguli, Mahurunga, Kivava, Libobe, Libobe 'B', Unguja, Namuhi, Ming'wena, Lipwidi, Mnyija na Mtama | 16 |
| | | Nanyumbu | Mbangala Mbuyuni, Marumba, Makanya, Lukula, Chungu, Lukwika, Chimika, Mpombe, Mchenjeuka, Nakopi, Chilunda, Mkumbaru na Lumesule | 13 |
| 3. | Morogoro | Gairo | Mamvisi, Lukando, Chanjale, Kumbulu, Mkobwe, Lufikiri, Chagongwe, Chingholwe, Ikwamba, Idibo, Masenge, Lukinga, Ihenje, Kinyolisi, Nongwe na Italagwe | 16 |
| | | Morogoro | Madamu, Luholole, Kivuma, Kibangile, NigeKifindike, Tawa na Lundi | 8 |
| | | Mlimba | Mkangawalo, Isago na Luvirikila | 3 |

| Na. | Mkoa | H/Wilaya | Kijiji | Idadi |
|---|---|---|---|---|
| 4. | Tabora | Nzega | Mogwa, Kilino, Kidete, Uduka, Kabanga, Isagenhe, Mbutu, Idubula, Kadoke, Kakulungu, Nkindu, Kishili, Milambo Itobo, Ikindwa, Nawa, Nyamalangwa, Bulende, Iboja, Bulambuka, Sigili, Chaming'hwa, Ilagaja, Chamipulu, Ngukumo, Kilabili, Mwakashanhala, Magukula na Kipilimuka | 28 |
| | | Sikonge | Kikungu, Chabutwa, Mkolye, Isunda, Kasandalala, Wankolongo, Mpombwe, Ibaya, Majojoro, Mwitikio na Mitowo | 11 |
| 5. | Iringa | Kilolo | Idete, Madege, Mbawi, Magome, Idegenda, Isanga, Ilutila, Ndengisivili, Lulindi, Kising'a, Kidumka, Udekwa, Ifuwa, Ukwega, Wotalisoli, Igunda, Nyanzwa, Msosa, Mgowelo, Kitowo, Ihimbo, Ikumbi Kitelawasi na Makungu | 24 |
| 6. | Dodoma | Bahi | Ilindi, Chiguluka, Nkhome, Mapanga, Zejele, Ikumbulu, Chifutuka, Chali, Isanga, Chali Makulu na Chali Igongo | 10 |
| | | Mpwapwa | Mzogole, Mzase, Kitati, Kidenge, Kingiti, Iyenge, Mgoma na Lukole | 8 |
| 7. | Lindi | Mtama | Madangwa, Njonjo, Pangatena, Hingawali, Nachunyu, Mtegu, Sudi, Mmumbu, Navanga na Kilimani | 10 |

| Na. | Mkoa | H/Wilaya | Kijiji | Idadi |
|---|---|---|---|---|
| 8. | Mtwara | Masasi | Chiwata, Chidya, Liloya, Mbemba Mpindimbi, Kanyimbi, Kachepa na Mapale | 8 |
| 9. | Pwani | Kisarawe | Chale, Boga, Mengwa, Ngongele Msegamo, Bembeza, Chang'ombe 'A' na Kibuta | 8 |
| | | Kibiti | Ruaruke 'A', Kikale na Mchungu | 3 |
| 10. | Mwanza | Misungwi | Busongo, Gulumungu, Lukanga, Ng'obo Ikungumhulu, Kabale, Mwamboku na Nyashitanda | 8 |
| 11. | Mbeya | Mbeya | Shitete, Shisonta, Itete, Shizingo, Ilindi, Idiwili, Mkuyuni, Itambalila, Shamwengo, Mbonile, Iyawaya, Pashungu na Iwowo | 13 |
| 12. | Tanga | Muheza | Mindu, Lunguza, Mkuzi, Mgome, Mpapayu, Ubembe, Misongeni na Enzi | 8 |
| | | Kilindi | Vyadigwa | 1 |
| 13. | Manyara | Mbulu | Murkuchida, Endamilay, Endalat na Yaeda Chini | 4 |
| | | Kiteto | Kinua, Ngipa, Ndirigishi, Krash, Taigo, Loltepes, Engusero Sidan, Ndotoi, Laiseri, Lerugu, Kiperesa, Engusero, Nasetani, Songambele, Nhati, Orikine, Magungu, Emarti, Sunya na Asamato | 20 |
| 14. | Kagera | Kyerwa | Masheshe | 1 |
| 15. | Simiyu | Busega | Nyamatembe, Manala, Badugu, Busami, Mwaniga, Shigala na Lwangwe | 7 |
| **JUMLA** | | | | **253** |